



## **SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

### **HOTUBA YA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI**

**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA (MBM)**

### **KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.**



**Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi akiwa na Uongozi wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na Viongozi wengine wa Serikali katika Maadhimisho ya Kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani tarehe 1/5/2021 katika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul-wakil Kikwajuni Zanzibar.**

**Mei, 2021**

## YALIYOMO

YALIYOMO.....	1
VIFUPISHO VYA MANENO.....	3
1. UTANGULIZI.....	5
2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI.....	8
3. MUHTASARI WA MATUMIZI NA MAPATO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.....	9
3.1 MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021.....	10
3.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU.....	11
3.2.1 PROGRAMU KUU PA0701: KUSIMAMIA HUDUMA NA KURATIBU SHUGHULI ZA MHESHIMIWA RAIS NA KUIMARISHA MAWASILIANO IKULU.....	11
3.2.2 PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE.....	19
3.2.2.1 Programu ndogo: SA070201: Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha.....	19
3.2.2.2 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini.....	21
3.2.2.3 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini.....	23
3.2.3 PROGRAMU KUU PA0703: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI.....	25
3.2.3.1 Programu ndogo SA070301: Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.....	25
3.2.3.2 Programu Ndogo: SA070302: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika.....	28
3.2.3.3 Programu Ndogo SA070303: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.....	30
3.2.4 PROGRAMU KUU PA0704: KUIMARISHA UWEKEZAJI NA SHUGHULI ZA SERIKALI KIKANDA NA KIMATAIFA.....	32
3.2.4.1 Programu ndogo SA070401: Maendeleo ya Ukuwaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji.....	32
3.2.4.2 Programu Ndogo SA070402: Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.....	36
3.2.4.3 Programu ndogo SA070403: Uratibu wa Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi.....	37
3.2.5 PROGRAMU KUU PA0705: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI.....	44
3.2.5.1 Programu ndogo SA070501: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara.....	44
3.2.5.2 Programu ndogo SA070502 Utawala na Uendeshaji.....	48
3.2.5.3 Programu ndogo SA070503: Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba.....	50
MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022.....	52
HITIMISHO.....	53

<b>VIAMBATANISHO</b> .....	55
<b>Kiambatanisho Nambari 1.</b> .....	55
<b>PROGRAMU KUU NA NDOGO ARKUU</b> .....	55
<b>Kiambatanisho Nambari 2.</b> .....	56
<b>MUHTASARI WA UPATIKANAJI WA FEDHA JULAI 2020 HADI MACHI, 2021</b> .....	56
<b>Kiambatanisho Nambari 3.</b> .....	57
<b>MUHTASARI WA MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI, 2021</b> .....	57
<b>Kiambatanisho Nambari 4.</b> .....	58
<b>UTOAJI WA MIKOPO YA MFUKO WA UWEZESHAJI KUANZIA JULAI 2020 HADI MACHI, 2021</b> .....	58
<b>Kiambatanisho nambari 5.</b> .....	59
<b>MCHANGANUO WA UTOAJI WA MIKOPO KWA MAKUNDI MAALUM 2020/2021</b> .....	59
<b>Kiambatanisho Nambari 6.</b> .....	61
<b>MAREJESHO YA MIKOPO MFUKO WA UWEZESHAJI KUANZIA JULAI 2020 HADI MACHI, 2021</b> .....	61
<b>Kiambatisho Nambari 7.</b> .....	62
<b>MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022</b> .....	62
<b>Kiambatanisho Nambari 8.</b> .....	63
<b>MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022</b> .....	63

## **VIFUPISHO VYA MANENO**

ADB	African Development Bank (Benki ya Maendeleo ya Afrika)
AfCTA	African Continental Free Trade Area (Vikwazo visivyokua vya Ushuru Barani Afrika).
CHODAW-Z	Conservation, Hotel, Domestic and Allied Workers Union (Umoja wa Wafanyakazi wa Mahoteli na Majumbani).
COMESA	Common Market for Eastern and Southern Afrika (Soko la Pamoja la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika).
EAC	East Africa Community (Jumuiya ya Afrika Mashariki).
ILO	International Labour Organization (Shirika la Kazi Duniani)
IORA	Indian Ocean Rim Association (Jumuiya ya Nchi zilizopakana na Bahari ya Hindi).
NTB's	Non – Tariff Barriers (Vikwazo vya Biashara visivyo vya Ushuru).
MoU	Memorandum of Understanding (Mkataba wa Makubaliano)
MIRVAF	Marketing Infrastructure, Value Addition and Rural Financial services (Huduma ya Kuimarisha Miundombinu ya Masoko kuongeza thamani ya Mazao na Uimarishaji wa Huduma za Fedha Vijijini)
PPP	Public Private Partnership (Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi)
SADC	Southern African Development Community
SMT	Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
SMZ	Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.
SW	Subhanahu Wataala
TBC	Tanzania Broadcasting Corporation (Shirika la Habari Tanzania)
TEWUTA-Z	Telecommunication Workers Union of Tanzania Zanzibar

TUICO-Z	Tanzania Union of Industrial and Commercial Workers
UNDP	United Nations Development Program (Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo).
UNIDO	United Nations Industrial Development Organization (Shirika la Kimataifa la Maendeleo ya Viwanda)
UN WOMEN	The United Nations Entity for Gender Equality and Women Empowerment (Shirika la Umoja wa Mataifa la kuleta Usawa wa Kijinsia na kuwawezesha Wanawake).
ZAECA	Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi
ZAFICOWU	Zanzibar Financial, Industrial, Consultant and Commercial Workers Union
ZANEMA	Zanzibar Employers Association
ZAPSWU	Zanzibar Public Service Workers Union
ZASU	Zanzibar Sea farmers Union
ZATUC	Zanzibar Trade Union Congress
ZBC	Zanzibar Broadcasting Cooperation
ZIPA	Zanzibar Investment Authority (Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar)
ZRB	Zanzibar Revenue Board (Bodi ya Mapato Zanzibar)
ZSSF	Zanzibar Social Security Fund (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar)
ZUPHE	Zanzibar Union of Public and Health Employees
ZUSP	Zanzibar Urban Service Program (Mradi wa Kuimarisha huduma za Miji)

## **1. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika;** Naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**2. Mheshimiwa Spika;** Kwanza kabisa napenda kumshukuru Allah (S.W) kwa kutujaalia uhai na afya njema na kuweza kukutana tena kujadili Bajeti ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Kwa niaba ya Wafanyakazi wa Afisi napenda kukupongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Baraza hili tukufu katika Serikali ya awamu ya nane. Pia, nampongeza Naibu Spika Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Wenyeviti wa Baraza kwa kuendelea kulihudumia Baraza kwa weledi na kukusaidia katika kazi ya kuliongoza Baraza. Aidha, Nawapongeza Wajumbe wote kwa kuchaguliwa kushika nafasi hizi muhimu kwa Maendeleo ya jamii yetu. Kuchaguliwa kwetu kunaonesha imani ya Wananchi kuwawakilisha katika chombo hichi muhimu cha maamuzi, katika Serikali hii ya awamu ya nane. Dhamana iliyopo mbele yetu sasa ni kuwatumikia kwa dhati Wananchi tunaowawakilisha kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu.

**3. Mheshimiwa Spika;** Kwa niaba ya Wafanyakazi wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji napenda kuipongeza na kuishukuru Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake hodari na shupavu Mheshimiwa Shaaban Ali Othman, Naibu Mwenyekiti Mheshimiwa Sabiha Thani Filfil na Wajumbe wake wote pamoja na Makatibu wao kwa kuwa bega kwa bega na Afisi kwa kipindi chote na kuipa ushauri na miongozo ya kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Ni matumaini ya Afisi kuwa mtaendelea kutupa mashirikiano ya kufanikisha malengo, majukumu na kutekeleza kwa vitendo Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Dira 2050, Ahadi na Sera za Kitaifa, Kikanda na Kimataifa zenye nia ya kuwainua Wananchi Kiuchumi; kuzalisha ajira nchini, kuimarisha uwekezaji nchini ili kuiletea maendeleo nchi yetu. Vile vile, Pongezi maalum ziende kwa Mheshimiwa Miraji Khamis Mussa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Bajeti

kwa kuiongoza kamati yake kwa uaminifu, hekima na busara. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo.

**4. Mheshimiwa Spika;** Kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kushinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Ushindi huu unaashiria imani ya Wananchi kwake pamoja na Chama cha Mapinduzi. Pia, tunamkushukuru kwa kuendelea kuimarisha utawala bora nchini pamoja na busara zake, hekima, maarifa na miongozo anayoendelea kuitoa ambayo inatoa Dira ya kufikia maendeleo endelevu ya Zanzibar na Wananchi wake.

**5. Mheshimiwa Spika;** Kwa kipindi kifupi ameweza kutuonesha mwelekeo wa Utekelezaji wa Shughuli za Serikali za kuwaletea Maendeleo Wananchi pamoja na kusimamia imara utekelezaji wa Dira 2050 na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo ikiwemo kudumisha Amani na utulivu. Pia, namshukuru kwa kunichagua na kuniamini kuiongoza Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji; Naahidi mbele yako na mbele ya Baraza hili kuwa nitaendelea kusimamia imara majukumu yote aliyonikabidhi kwa kushirikiana na watendaji wenzangu.

**6. Mheshimiwa Spika;** Nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais kufuatia kifo cha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Hayati Maalim Seif Sharif Hamad. Ni matarajio yetu kwamba atafuata nyayo na kuziendeleza busara, fikra na uzalendo wa Marehemu Maalim Seif Shariff Hamad katika kusimamia umoja wa kitaifa, maendeleo ya nchi, haki, ustawi, mshikamano na maslahi ya Wazanzibari. Vile vile, nampongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kusimamia imara utekelezaji wa majukumu yote ya Serikali.

**7. Mheshimiwa Spika;** Naomba kuchukua nafasi hii kuwapa pole Wananchi wote wa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuondokewa na kiongozi wetu mpenzi Maalim Seif Sharif Hamad. Kifo cha kiongozi huyu kimeacha pengo kubwa kwa mustakbali wa Zanzibar katika kuimarisha mshikamano na uendelezaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Maalim Seif amefariki katika kipindi ambacho Zanzibar ina

muhitaji kupata mchango wake katika kuharakisha Maendeleo ya Zanzibar na kudumisha amani na usalama wa Nchi yetu. Hata hivyo, kazi ya Allah (S.W) haina makosa tunamuomba amuweke mahali pema peponi Amin. Wazanzibar tunaamini kilichokufa ni kiwiliwili lakini fikra, hekima, miongozo na mawazo yake bado yatabakia kuwa ni Dira ya kufikia Zanzibar yenye amani na maendeleo kwa kizazi cha sasa na kijacho.

**8. Mheshimiwa Spika;** Kwa niaba ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji natoa pole kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na Rais wetu mpendwa Hayati John Pombe Joseph Magufuli aliyefariki dunia tarehe 17 Machi, 2021 pamoja na aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Muhandisi Balozi John William Kijazi. Kifo cha Marehemu John Pombe Magufuli kimeleta pengo kubwa kwa maendeleo ya Tanzania na Afrika kwa ujumla.

**9. Mheshimiwa Spika;** Hayati Magufuli ameondoka wakati ambapo watanzania wanamuhitaji sana kupata busara na maelekezo yake ili kufikia Tanzania mpya. Hata hivyo ni matumaini ya wananchi kuwa marehemu Magufuli hakuwa akifanya kazi peke yake, viongozi wengine tutafuata nyayo zake na kuendeleza jitihada za kuleta maendeleo kwa kutumia utajiri wa rasilimali tulizobarikiwa nchini bila ya kutegemea misaada zaidi kutoka nje. Pia, nachukua fursa hii kuwapa pole wanafamilia na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu na Marehemu amlaze mahala pema peponi Amin.

**10. Mheshimiwa Spika;** Halkadhalika, nachukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kwa kumpokea kijiti Hayati Magufuli na kuwa Rais wa kwanza mwanamke wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Afrika Mashariki. Tunamuomba Mwenyezi Mungu katika utawala wake amuhifadhi, ampe moyo wa ushupavu, hekima, uadilifu, busara pamoja na ujasiri katika kutekeleza majukumu yake.

**11. Mheshimiwa Spika;** Nampongeza Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi Mhandisi Zena Ahmed Said kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo akiwa ni mwanamke wa kwanza kwa Zanzibar na Tanzania kushika nafasi kama hiyo. Hii inaonesha imani ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi ya kutekeleza ahadi ya kuzingatia jinsia katika uteuzi wake aliyoitoa wakati wa kampeni pamoja na kuthamini umahiri na mchango wa wanawake katika kuleta maendeleo ya nchi yetu. Kwa muda mchache aliochaguliwa Mhandisi Zena Ahmed Said ameweza kuudhihirishia umma kupitia utendaji wake kuwa **WANAWAKE WANAWEZA.**

**12. Mheshimiwa Spika;** baada ya utangulizi huo, sasa naomba uniruhusu niwasilishe utekelezaji wa Programu za Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

## **2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA AFISI YA RAIS KAZI UCHUMI NA UWEKEZAJI**

**13. Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji imeanzishwa kwa lengo la kusimamia masuala ya uwekezaji nchini; kusimamia utekelezaji wa Sheria na miongozo ya kazi; kuratibu upatikanaji wa ajira za staha hasa kwa Vijana; kuimarisha programu za kuwawezesha wananchi kiuchumi; kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa pamoja na mashirikiano na wazanzibar wanaoishi nje ya nchi; kuimarisha mashirikiano kati ya Sekta ya umma na Sekta binafsi pamoja na kusimamia Shughuli za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Afisi inatekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu 5 na Programu ndogo 14 **Kiambatanisho nambari 1 kinahusika.**

**14. Mheshimiwa Spika;** Utekelezaji wa Programu hizi umezingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025, Dira ya Maendeleo 2050, Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar pamoja na Mpango Mkakati wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji

### **3. MUHTASARI WA MATUMIZI NA MAPATO KWA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**15. Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Tatu Thamanini na Tisa, Laki Saba Sitini na Saba Eflu, Mia Tatu Hamsini na Nne** (Tshs. 14,389,767,354). Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Mbili Ishirini na Mbili, Laki Saba Tisini na Tano Eflu** (Tshs.4,222,795,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu; **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Sabini na Nane, Laki Tisa** (Tshs.1,478,900,000) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote;

**Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili Thamanini na Tano, Laki Moja Thalathini na Sita Eflu, Mia Tano na Arobaini na Nane** (Tshs.2,285,136,548) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba na Kumi, Laki Tatu Kumi na Tano Eflu, Mia Nne na Hamsini** (Tshs.1,710,315,450) kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Shughuli za Serikali Kikanda na Kimataifa na **Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Sita Tisini na Mbili, Laki Sita Ishirini Eflu, Mia Tatu Hamsini na Sita** (Tsh.4,692,620,356) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

**16. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Machi 2021, fedha zote zilizoingizwa ni **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Nne Kumi na Tisa, Laki Sita na Eflu Saba, Mia Saba Arobaini na Nane** (Tshs.7,419,607,748) ambayo ni sawa na asilimia Hamsini na Mbili (52%) ya utekelezaji wa Programu zote. Kati ya hizo **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Sitini na Mbili, Laki Nne Eflu Saba, Mia Moja Hamsini na Nane** (Tshs.2,462,407,158) zilitumika kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu sawa na asilimia

Hamsini na Nane (58%); **Shilingi Milioni Mia Sita Thalathini, Laki Tatu Thalathini na Tisa Eflu, Mia Mbili Thamanini** (Tshs.630,339,280) zilitumika kutekeleza Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote ambayo ni sawa na asilimia Arobaini na Mbili (42%) ya fedha kwa programu hiyo. **Shilingi Milioni Mia Sita Arobaini na Mbili, Thalathini na Tatu Eflu, Mia Mbili Sitini na Tisa** (Tshs.642,033,269) zilitumika kwa kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ni sawa na asilimia Ishirini na Nane (28%);

**Shilingi Milioni Mia Sita Tisini na Tisa, Laki Tano Ishirini na Moja Eflu, Mia Tisa Thalathini na Moja** (Tshs.699,521,931) zilitumika kwa kutekeleza Programu ya Kuimarisha Uwekezaji na Shughuli za Serikali Kikanda na Kimataifa sawa na asilimia Arobaini na Moja (41%); **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tisa Thamanini na Tano, Laki Tatu na Eflu Sita, Mia Moja na Kumi** (Tshs.2,985,306,110) zilitumika kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji sawa na asilimia Sitini na Nne (64%) ya fedha za Programu hiyo. Mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopatikana Julai 2020 hadi Machi 2021 kwa Programu Kuu na ndogo Kiambatanisho nambari 2 kinahusika.

### **3.1 MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

**17. Mheshimiwa Spika,** Afisi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ilitarajiwa kukusanya mapato ya **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Sabini na Nane, Laki Tano Hamsini na Tano Eflu** (Tshs.2,078,555,000) kutokana na Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi. Hadi Mwezi Machi 2021, Afisi kupitia Kamisheni ya Kazi, Idara ya Ajira, Idara ya Usalama na Afya Kazini na Idara ya Ushirika ilifanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi Milioni Mia Sita Sitini na Saba, Laki Saba Thamanini na Saba Eflu, Mia Saba Ishirini na Saba** (Tsh.667,787,727) kutokana na Ada za Usajili, Ada ya Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika na Vibali vya Kazi ambayo ni sawa na asilimia

Thalathini na Mbili (32%) ya Makadirio ya Makusanyo (Kiambatanisho nambari 3 kinahusika).

## **3.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

### **3.2.1 PROGRAMU KUU PA0701: KUSIMAMIA HUDUMA NA KURATIBU SHUGHULI ZA MHESHIMIWA RAIS NA KUIMARISHA MAWASILIANO IKULU.**

**18. Mheshimiwa Spika;** Programu hii inasimamia shughuli zote za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikiwemo masuala ya kuimarisha Mawasiliano baina ya Ikulu na Wananchi.

**19. Mheshimiwa Spika;** Itakumbukwa kuwa mnamo Mwezi Novemba mwaka 2020, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi alichaguliwa na Wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na aliapishwa rasmi kushika wadhifa huo tarehe 2 Novemba 2020. Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliahidi kuongoza nchi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar yenye kuisitiza kufuata misingi ya usawa, umoja na maridhiano na kwamba maendeleo ya Zanzibar ni muhimu zaidi kuliko tofauti zetu.

**20. Mheshimiwa Spika;** Rais Dkt. Mwinyi alisisitiza kuwa uchaguzi umekwisha na kazi iliyo mbele yetu ni kuijenga nchi ambapo kila mmoja wetu ana wajibu wa kushiriki katika mchakato huo. Pia, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anaendelea kuongoza nchi kwa kufuata misingi ya utawala bora ikiwemo kuimarisha utoaji wa huduma mbali kwa wananchi, uwajibikaji na ubunifu.

**21. Mheshimiwa Spika;** Katika hotuba yake aliyoitoa tarehe 11 Novemba 2020 wakati wa uzinduzi wa Baraza la kumi la Wawakilishi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alisisitiza ahadi yake aliyoiahidi wakati wa kampeni ya kuijenga Zanzibar mpya

kwa kuimarisha uchumi wa kisasa wa buluu (Blue Economy) ambao unafungamanisha kwa pamoja sekta za uvuvi, ufugaji samaki, ujenzi wa viwanda vya kusindika samaki, ukulima wa mwani, uchimbaji wa mafuta na gesi, uendelezaji wa bandari na mambo kadhaa yanayohusiana na baharí. Ili kulitekeleza hilo Mheshimiwa Rais ameunda Wizara Maalum inayoshughulikia masuala ya Uchumi wa Buluu. Aidha, alielezea namna atakavyoshirikiana na sekta binafsi katika kukuza na kuimarisha sekta ya utalii, ambayo hivi sasa ndio muhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar.

**22. Mheshimiwa Spika;** Katika hotuba yake hiyo, alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Nane ina dhima ya kuwaunganisha wananchi na kuondokana na aina zote za ubaguzi na kwamba uteuzi wa viongozi wa Serikali utafanywa kwa kuzingatia uwezo wa mtu kitaaluma, uwajibikaji, uaminifu na uzalendo. Katika kuhakikisha kwamba anatimiza ule usemi maarufu wa Kiswahili usemao **“Ada ya Mja Kunena Uungwana ni Vitendo”**, Rais wa Zanzibar tarehe 6 Disemba 2020, alimteua Hayati Maalim Seif Sharif Hamad, kutoka Chama cha ACT Wazalendo kuwa Makamo wa kwanza wa Rais wa Zanzibar. Uamuzi huo ilikuwa ni hatua muhimu ya kuwathibitishia Wananchi wa Zanzibar na dunia nzima dhamira yake ya kweli ya kuwaunganisha wananchi wa Zanzibar pamoja na kutekeleza yale yote mengine aliyoyaahidi.

**23. Mheshimiwa Spika;** Katika kutekeleza majukumu yake, Mheshimiwa Rais amefanya mambo mbali mbali yakiwa ni pamoja na uteuzi wa viongozi na watendaji, kufanya ziara za kikazi, kufanya mikutano na wadau mbali mbali Ikulu na nje ya Ikulu na kuhudhuria matukio makuu kama vile Sherehe za miaka 57 ya Mapinduzi na shamrashamra za uzinduzi wa miradi. Vile vile, alishiriki hafla za mazishi ya aliyekuwa Makamo wa Kwanza wa Rais Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad na mazishi ya Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**24. Mheshimiwa Spika;** Mheshimiwa Rais alifanya teuzi za viongozi mbali mbali na baadae kuwaapisha. Walioteuliwa na baadae kuapishwa ni pamoja na wasaidizi wake wakuu Makamu wa Kwanza

wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Vile vile, aliwateua na kuwaapisha Mawaziri wa Serikali, Wakuu wa Mikoa, Makatibu wakuu na Naibu Makatibu wakuu pamoja na Wakuu wa Wilaya. Katika hotuba yake alipowaapisha Waheshimiwa Mawaziri na Makatibu wakuu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alitoa maagizo maalum ambayo yalihitaji kutekelezwa na viongozi na watendaji hao.

**25. Mheshimiwa Spika;** Miongoni mwa maagizo yaliyotolewa alimtaka kila Waziri kuijua Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara anayoiongoza kwa kuitembelea, kutengeneza mpango kazi na bajeti kwa kutumia Ilani ya CCM, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Maagizo aliyoyatoa katika Hotuba yake wakati alipokuwa akifungua Baraza la Wawakilishi na ahadi zake wakati wa kampeni. Sambamba na hilo, Mawaziri walitakiwa wapate maoni ya Wadau kuhusiana na huduma wanazozitoa kwa wananchi. Vile vile, Waheshimiwa Mawaziri walitakiwa kutembelea miradi yote ya Wizara kwa kuangalia ubora, utaratibu wa zabuni, malipo yaliyofanyika na muda wa kumaliza mradi. Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameweka utaratibu maalum wa kufuatilia utekelezaji wa Maagizo hayo aliyoyatoa kwa Waheshimiwa Mawaziri kwa kuweka vikao vya pamoja na Watendaji wa Wizara hizo.

**26. Mheshimiwa Spika;** Vile vile, Waheshimiwa Mawaziri walitakiwa kusimamia vyema suala la uwajibikaji wa watendaji kwa kuhakikisha kuwa kila mtu atawajibika kwa kazi aliyopewa ili kuona kuwa huduma zote zinatolewa kwa ufanisi na haraka kama inavyohitajika na pia kuhakikisha kuwa haki za wafanyakazi na wananchi wote kwa jumla zinatolewa. Pia, Mheshimiwa Rais aliwaagiza Mawaziri kusimamia suala la utawala bora kukomesha rushwa, ubadhirifu wa mali ya umma, wizi na kusimamia ukusanyaji wa mapato yote ya Serikali na hasa yale yanayokusanywa na TRA na ZRB. Mheshimiwa Rais ameanza kuchukua hatua mbali mbali kwa Viongozi na Watendaji wazembe ikiwemo kuwasimamisha kazi. Aidha, aliwataka viongozi hao kuwa wabunifu na kuondoa urasimu katika Ofisi wanazoziongoza pamoja na kuwa wepesi wa kutoa mapendekezo pale watakapoona

kuna haja ya kubadilisha sheria ambazo zitaonekana kuwa ni kikwazo katika kutekeleza majukumu yao.

**27. Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha utoaji wa habari na taarifa mbali mbali kwa wananchi juu ya utekelezaji wa majukumu ya Serikali, Rais wa Zanzibar aliwataka viongozi aliowateua kuweka utaratibu wa utoaji wa taarifa kwa kazi wanazozifanya kwenye vyombo vya habari ili umma ujue mafanikio na changamoto za Wizara zao na kama kuna changamoto, waeleze namna ya kukabiliana na changamoto hizo. Vile vile, aliwataka kusikiliza changamoto za watu na kutatua kero zao, kuweka utaratibu wa kusikiliza malalamiko ya watu. Pamoja na hayo, aliwataka kuzingatia usafi kwenye majengo ya Ofisi zao. Katika kutekeleza hilo, Idara ya Mawasiliano Ikulu imeweka utaratibu maalum wa kusikiliza kero za Wananchi na kuzifanyia kazi.

**28. Mheshimiwa Spika;** Ikiwa ni muendelezo wa mikakati yake ya kuimarisha uwekezaji nchini, Mheshimiwa Rais amehudhuria na kushuhudia utiaji saini wa Mpango Mkuu wa Upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Bandari Shirikishi "Multipurpose Fish Port" katika eneo la Mpiga Duri Unguja na Mkoani Pemba pamoja na Mradi wa Ufuaji wa Umeme kwa nishati ya gesi baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Makampuni ya "Intertorco Group" na "Monitor Power System. Vile vile, alishuhudia utiaji saini wa hati ya maelewano (MoU) inayohusu Mpango Mkuu wa Ujenzi wa Bandari ya Mangapwani unaojumuisha bandari ya mizigo, uvuvi, mafuta na gesi asilia, chelezo na mji wa kisasa baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Mamlaka ya uwekezaji ya Oman. Matukio haya yalifanyika Ikulu, Zanzibar tarehe 29 Januari 2021 na tarehe 4 Februari 2021.

**29. Mheshimiwa Spika;** Miongoni mwa shughuli alizozifanya Mheshimiwa Rais nje ya Ikulu ni pamoja na kuhudhuria mikutano ya wadau wa makundi tofauti ambapo alikutana na wadau wa Sekta ya Elimu, Mji Mkongwe, Wanaharakati na taasisi zinazohusika na masuala ya udhalilishaji, Wafanyakazi wa Sekta ya Afya, Sekta ya Habari na wadau wa Sekta binafsi. Mikutano hiyo kwa ujumla ilileta matokeo chanya kwa mustakbali wa maendeleo ya Zanzibar ambapo hatua kadhaa zimechukuliwa kama vile kuundwa kwa Kamati maalum

ya kushughulikia changamoto za Mji Mkongwe, kuanza kulipwa malimbikizo ya posho za watumishi wa Sekta ya Afya, kupitishwa uamuzi wa kuanzishwa Mahakama Maalum dhidi ya vitendo vya udhalilishaji na kufanyika Kongamano la kutathmini Sera ya Elimu Zanzibar.

**30. Mheshimiwa Spika;** Mheshimiwa Rais anaendelea kufanya ufuatiliaji wa Programu na Miradi mbali mbali ya Maendeleo kujiridhisha juu ya utekelezaji wake na kuweza kubaini changamoto za kiutendaji zinazotokea katika kutekeleza kwa ufanisi Programu hizo. Pia, hutoa maagizo ya kutatuliwa kwa haraka changamoto hizo. Ufuatiliaji huu unajumuisha ziara za kushtukiza na za kawaida. Mheshimiwa Rais wa Zanzibar alifanya ziara za kushtukiza katika Shirika la Bandari Zanzibar, Hospitali kuu ya Mnazi Mmoja, Miradi ya ZUSP na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA). Ziara hizo kwa zimeleta mabadiliko makubwa kwa kuongeza kasi na ufanisi katika maeneo yaliyotembelewa.

**31. Mheshimiwa Spika;** Kufuatia ziara hizo, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto imefanya mabadiliko makubwa katika Sekta ya Afya kufuatia ziara hiyo ambako hivi sasa wafanyakazi wote wanaweza kutambuliwa kutokana na kuvaa sare maalum na kuweka alama za utambulisho wao, huduma zimeimarika katika vitengo vyote ingawa bado kazi zaidi inahitaji kufanyika katika kuimarisha huduma. Katika ziara aliyoifanya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA), Mheshimiwa Rais aliwaahidi wafanyakazi wa taasisi hiyo kuondoa changamoto zote zinazoathiri utekelezaji wa majukumu yao. Aidha, aliwaahidi kufanya kazi nao kwa karibu zaidi ili kuleta mafanikio yaliyokusudiwa.

**32. Mheshimiwa Spika;** Kwa upande wa ziara kwenye Mradi wa Huduma za Miji (ZUSP), Kamati maalum iliundwa kufuatilia mradi huo. Matokeo ya ziara hiyo ni kwamba kasi ya utekelezaji wa mradi imeongezeka, wananchi wa Kibele waliokuwa na madai ya fidia kutokana na kujengwa jaa la kisasa kwenye eneo lao wamelipwa fedha zao. Vile vile, Mheshimiwa Rais alifanya ziara katika Maeneo tofauti ya Miji kuangalia hali ya Usafi wa Miji. Kiukweli hajaridhishwa

na hatua za Manispaa zetu wanavyofanya katika kusimamia Usafi wa maeneo yao. Mheshimiwa Rais aliwaagiza Waheshimiwa Wakuu wa Mkoa na Wilaya kulisimamia hilo na hivi sasa hali ya usafi imeimarika zaidi katika mji wa Zanzibar. Vile vile, Mheshimiwa Rais alifanya ziara kisiwani Pemba kwenda kufungua rasmi jengo la ZSSF, na kuwashukuru wananchi wa Pemba kwa kumchagua kuwa Rais wa Zanzibar kwenye Uchaguzi Mkuu uliofanyika Mwezi Oktoba mwaka 2020. Pia, alitembelea mradi wa nyumba za maafa na kufungua msikiti uliopo Gombani.

**33. Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha mashirikiano ya Kikanda na Kimataifa, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anaendele kupokea wageni mashuhuri mbali mbali katika Ikulu ya Zanzibar wakiwemo Viongozi wa Serikali, Mabalazi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa na Makampuni ya watu binafsi ya ndani na nje ya nchi. Wageni hawa wameridhishwa na utekelezaji wa kazi na uimarishaji wa Utawala Bora wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na kuahidi kuimarisha mashirikiano baina ya Zanzibar na Nchi hizo.

**34. Mheshimiwa Spika;** Mikutano hiyo imeimarisha uhusiano na diplomasia baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wawakilishi wa Serikali waliomtembelea. Vile vile, uhusiano na Mashirika na Taasisi hizo umeimarika na kutoa fursa mpya ya kuangalia namna ya kuendeleza ushirikiano katika sekta tafauti za maendeleo na ustawi wa jamii. Aidha, kwa upande wa wageni kutoka taasisi za uwekezaji na wafanyabiashara, tayari baadhi ya taasisi hizo zimeonesha dhamira ya kutaka kutumia fursa za uwekezaji zilizopo Zanzibar kuja kuwekeza katika miradi tofauti ikiwemo ya uanzishaji wa viwanda na uzalishaji wa nishati ya umeme.

**35. Mheshimiwa Spika;** Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi tarehe 08/04/2020 alimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika SADC

nchini Msumbiji. Mkutano huo ulihudhuriwa na Viongozi mbali mbali akiwemo Rais wa Msumbiji Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi ambaye ni Mwenyekiti wa SADC. Wakuu wa Nchi walijadili hali ya ulinzi na usalama katika Ukanda wa Jumuiya ya SADC; mashambulizi na hali ya uvunjifu wa amani katika Pwani ya Msumbiji na namna nchi hizo zitavyoshirikiana katika kupambana na kuondoa vitendo vya ugaidi hasa katika jimbo la Cabo Delgado nchini Msumbiji. Aidha, wamelaani vitendo hivyo na kutoa pole kwa Wananchi wa Msumbiji na wameahidi kuunga mkono jitihada za kiusalama za kurudisha amani ya kweli katika eneo hilo ili kuendeleza shughuli zote za maendeleo katika nchi.

**36. Mheshimiwa Spika;** Juhudi maalum zimeendelea kuchukuliwa katika kuimarisha Idara ya Mawasiliano Ikulu. Idara hii imeendelea na utoaji wa taarifa zake kupitia mitandao ya kijamii ya facebook, WhatsApp, twitter, instergram na mengineyo. Tathmini ya karibuni imeonesha kuwa watu wengi ndani na nje ya Zanzibar hufuatilia taarifa za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi na hasa shughuli zake zinazorushwa moja kwa moja yaani "Live" kupitia mitandao hiyo. Kutokana na maendeleo haya kwa sasa hata ndugu zetu waliopo nje ya nchi wamekua mstari wa mbele kufuatilia taarifa hizi na kuweza kutoa maoni yao kupitia mitandao hiyo kitu ambacho hakikuwepo hapo awali.

**37. Mheshimiwa Spika;** Ili kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais Ikulu mwezi Februari mwaka huu imeanzisha Mfumo mpya wa Mawasiliano unaojulikana kama Sema na Rais Mwinyi (SNR-MWINYI). Mfumo huu unaotumia njia za kisasa za Mawasiliano unasimamiwa na mwenyewe Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. SNR- MWINYI umeongeza ufanisi katika suala zima la Mawasiliano baina ya Rais, Wananchi na Serikali kwa jumla.

**38. Mheshimiwa Spika;** Mfumo wa SNR-MWINYI umesaidia kutambua kwa haraka maeneo yenye changamoto kubwa kwa wananchi na kuyafanyia kazi; kuharakisha ufumbuzi wa changamoto za wananchi; umewarahisishia wananchi njia za kuwasilisha kero zao

Serikalini; umepunguza gharama za ufuatiliaji na umewafanya watendaji kutekeleza majukumu yao kwa wakati na kwa ufanisi. Pia, umeongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya Serikali, umesaidia kubainisha mianya ya rushwa, uzembe na ubadhirifu, umewafanya watendaji kuwa makini zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao na kupunguza gharama za shughuli nyingi zilizokuwa zikifanywa kama vile kufuatilia kero za wananchi katika ngazi za chini.

**39. Mheshimiwa Spika;** Wananchi wanaendelea kupata matukio na habari zinazohusu shughuli za Mheshimiwa Rais kupitia machapisho, majarida na vipindi vinavyorushwa hewani. Idara ya Mawasiliano ya Mheshimiwa Rais Ikulu imefanikiwa kuchapisha kalenda ya Ikulu kopi 5,500 na kusambazwa katika taasisi za Serikali na taasisi binafsi pamoja na kuchapisha Kipeperushi kilichobeba nukuu 12 za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi ambacho kimesambazwa kwa wananchi waliotembelea banda la maonesho la Ikulu wakati wa shamra shamra za Sherehe za Mapinduzi.

**40. Mheshimiwa Spika;** Idara ya Mawasiliano Ikulu imetayarisha na kurusha vipindi 15 vya televisheni na vipindi 11 vya redio ambavyo vilielezea utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na utekelezaji wa ahadi za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambazo huzitoa katika nyakati tofauti. Vipindi hivyo vilitayarishwa na kurushwa kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC). Vile vile, Ziara za utayarishaji wa vipindi vijijini pamoja na kuonesha sinema zinazowahamasisha wananchi katika harakati za maendeleo nchini zilifanyika. Hata hivyo, shughuli hizi zilisimama kwa muda kutokana na changamoto ya maradhi ya CORONA na shughuli za uchanguzi.

**41. Mheshimiwa Spika;** Mheshimiwa Rais wa Zanzibar mnamo tarehe 1 Mei, 2021 alihudhuria kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani kilichofanyika Ukumbi wa Sheikh Idriss Abdul-wakil Kikwajuni Zanzibar. Mheshimiwa Rais katika hotuba yake aliwapongeza Wafanyakazi wa Sekta Umma na Sekta ya Binafsi na kusisitiza dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa haki na maslahi ya

wafanyakazi wote zinazingatiwa na zinapatikana ikiwemo mazingira mazuri ya kufanya kazi. Kuhusu suala la kikokotoa kama alieleza kuwa ni changamoto kwa wafanyakazi wanaostaafu na ameahidi kulifanyia kazi suala hilo.

**42. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi inakusudia kuendelea kusimamia huduma za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Kusimamia shughuli za Viongozi Wakuu Wastaafu; Kuimarisha majengo ya Ikulu na Kuimarisha Mawasiliano baina ya Wananchi na shughuli zinazofanywa na Mheshimiwa Rais.

**43. Mheshimiwa Spika;** Ili Program Kuu ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Tano, Laki Nane Thamanini na Saba Eflu** (Tshs.5,005,887,000) ambapo **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Tisa Hamsini na Tatu, Laki Tisa Sabini na Nne Eflu** (Tshs.3,953,975,000) kwa ajili ya utekelezaji wa Programu ndogo ya Kusimamia Huduma na Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Hamsini na Moja, Laki Tisa Kumi na Mbili Eflu** (Tshs.1,051,912,000) kwa ajili ya Programu Ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi kwa matumizi ya kawaida na maendeleo.

### **3.2.2 PROGRAMU KUU PA0702: USIMAMIZI WA SHERIA ZA KAZI, UKAGUZI KAZI NA KAZI ZA STAHA KWA WOTE.**

#### **3.2.2.1 Programu ndogo: SA070201: Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha**

**Lengo kuu:** Kupunguza kiwango cha ukosefu wa Ajira kwa Vijana

**44. Mheshimiwa Spika;** Katika kuratibu upatikanaji wa Ajira nchini katika Sekta Binafsi, Programu imeratibu upatikanaji wa Ajira 1,272 (Wanaume 603 na Wanawake 669) katika Sekta Binafsi ndani ya Nchi

katika sekta za hoteli, viwanda, skuli binafsi na ulinzi. Aidha, Programu kwa kushirikiana na Taasisi za Wakala Binafsi wa Ajira imeratibu upatikanaji wa Ajira 842 (Wanaume 59 na Wanawake 783) nje ya nchi ikiwemo Oman, Qatar na Dubai kwa kazi za ulezi wa watoto, udereva, ulinzi, upishi na kazi za nyumbani.

**45. Mheshimiwa Spika;** Pia, imefanikiwa kutoa mafunzo ya vitendo kwa vijana ili waweze kujajiri na kuajirika na kuendelea kuratibu Programu ya Mafunzo Kazi Awamu ya Pili kwa vijana 106 (Wanawake 35 na Wanaume 71) katika fani ya hotelia kwa kipindi cha miaka miwili.

**46. Mheshimiwa Spika;** Vile vile, imeratibu mafunzo ya muda mfupi ya ujuzi (Modular Apprenticeship) kwa vijana wasio na ajira, ujuzi na hawatambuliwi na Mfumo wa Elimu (NEET). Programu hii imewanufaisha vijana 100 ambapo vijana 71 wamesomea fani ya ufundi wa Mafriji na Vipoza hewa katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume na vijana 29 wamesomea fani ya Useremala katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Mwanakwerekwe na Skuli ya Sekondari ya Ufundi ya Mikunguni.

**47. Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za soko la ajira, Programu imesajili Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira, baada ya kuufanyia marekebisho. Mfumo huo kwa sasa una uwezo wa kutangaza fursa za Ajira pale zinapopatikana hasa katika Sekta Binafsi. Aidha, maombi ya wanaotarajia kwenda kufanya kazi nje ya nchi yataombwa kupitia mtandaoni pamoja na maombi ya Uwakala Binafsi wa Ajira. Mfumo huo unajulikana kwa jina la **zanlmis.kaziuwekezajismz.go.tz.**

**48. Mheshimiwa Spika;** Programu ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha kwa mwaka wa fedha 2021/2022, imepanga kuwawezesha na kuelimisha jamii juu ya upatikanaji wa ajira za staha kwa kutangaza nafasi na fursa za ajira zitakazopatikana kupitia Mfumo wa Taarifa za Soko la Ajira na Vyombo vya Habari; itaimarisha Mfumo wa Taarifa za Ajira; itaimarisha mashirikiano na wadau wa nje na ndani katika kutafuta fursa za ajira kwa vijana; itatoa mafunzo kwa watafuta

kazi juu ya kujiajiri na kuajirika; itaendelea kusimamia Program ya mafunzo kazi kwa wanagenzi na Programu ya Vijana wasio katika elimu wala ajira (NEET).

**49. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka 2021/2022, naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku na fedha za maendeleo ya jumla ya **Shilingi Milioni Mia Sita na Ishirini** (Tshs. 620,000,000) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na maendeleo.

### **3.2.2.2 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini.**

**Lengo Kuu:** Kuimarisha masuala ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi.

**50. Mheshimiwa Spika;** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Usalama na Afya Kazini na inasimamia utekelezaji wa Sheria Na. 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini.

**51. Mheshimiwa Spika;** Programu imefanya usajili wa sehemu za kazi 118 (85 Unguja na 33 Pemba) ili kuzitambua na kuweka taarifa zao kwenye daftari la usajili wa sehemu za kazi. Ukaguzi huu unaturahisishia kutambua mapema mazingira ya kazi, hatari zinazoweza kutokea katika sehemu hizo na hatimae kutoa ushauri na maelekezo yanayofaa kabla ya kutokea tatizo.

**52. Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha masuala ya usalama na afya kazini, Afisi imefanya ukaguzi wa sehemu za kazi 157 (106 Unguja na 51 Pemba) za umma na binafsi ili kuangalia hali ya usalama na afya katika maeneo hayo. Ushauri ulitolewa juu ya kurekebisha kasoro zilizobainika. Ufuatiliaji uliofanywa baada ya ukaguzi umeonesha kuwa kasoro nyingi zimerekebishwa baada ya kufuatwa ushauri uliotolewa.

**53. Mheshimiwa Spika;** Pia, imefanya uchunguzi wa matukio ya ajali na maradhi yatokanayo na kazi katika sehemu (5) za kazi ambazo ziliripotiwa Idarani kutokea kwa ajali hizo wakati wafanyakazi wakiendelea na kazi. Wafanyakazi 2 walifariki na wengine walipoteza viungo kama vile miguu na vidole. Baadhi walipata maumivu kwenye

maeneo tofauti ya miili yao. Aidha, ipo ajali ambayo iliteketeza kiwango kikubwa cha mali za sehemu za kazi (Tui Blue) lakini hakuna mtu aliyejeruhiwa kwenye ajali hiyo.

**54. Mheshimiwa Spika;** Programu imeandaa na kurusha hewani vipindi vitatu (3) vya redio na vipindi vinne (4) vya televisheni kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC). Vile vile, imetoa mafunzo kwa Wafanyakazi kwenye Taasisi mbali mbali wakati Wafanyakazi wakiendelea na shughuli zao za kawaida ambayo yalilenga kuelimisha wafanyakazi na waajiri juu ya mazingira bora ya kufanya kazi na kuhakikisha wafanyakazi wapo salama muda wote wanapokuwa katika maeneo ya kazi.

**55. Mheshimiwa Spika;** Programu ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini kwa mwaka wa fedha 2021/2022, itaendelea kutekeleza Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini kwa ajili ya kuimarisha mazingira bora ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi; itaimarisha Mfumo wa ukaguzi wa hali ya Usalama na Afya Kazini kwa kuwajengea uwezo wakaguzi wake; itafanya ukaguzi wa sehemu za kazi 240 na kufanya usajili wa sehemu za kazi 120; itatoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi katika sehemu za kazi; itaelimisha wawakilishi 300 wa usalama na afya kazini (150 Sekta ya Umma na 150 Sekta Binafsi) Unguja na Pemba; itaimarisha mashirikiano na uratibu wa masuala ya usalama na afya kazini na kutoa taaluma juu ya hatari zinazoweza kutokea katika sehemu za kazi na namna ya kukabiliana nazo na itakuza uelewa wa usalama na afya kazini kwa kupitia vyombo vya habari (vipindi 24).

**56. Mheshimiwa Spika;** Ili Programu ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku ya **Shilingi Milioni Mia Moja na Ishirini** (Tshs.120,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

### **3.2.2.3 Programu Ndogo SA070202: Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini.**

**Lengo Kuu:** kuhakikisha kunakuwepo Utekelezaji Mzuri wa Sheria za Kazi.

**57. Mheshimiwa Spika;** Kamisheni ya Kazi imeundwa kwa Sheria ya Ajira Nam. 11 ya 2005 ikiwa na lengo la kusimamia viwango vya kazi vya kitaifa na majadiliano ya pamoja ya kazi ili kuhakikisha kunakuwepo utekelezaji mzuri wa Sheria za Kazi katika sekta binafsi kwa hapa Zanzibar. Miongoni mwa majukumu yake ni kufanya ukaguzi kazi kwa taasisi za sekta binafsi, kusimamia Ajira za Wafanyakazi wa kigeni, kuthibitisha Mikataba ya Wafanyakazi wazalendo na wageni na kuimarisha mahusiano mema kati ya waajiri na waajiriwa sehemu za kazi.

**58. Mheshimiwa Spika;** Programu imefanya ukaguzi kazi kwa Taasisi 152 (Unguja 126 na Pemba 26) ili kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Sheria za Kazi kwa taasisi zote. Vile vile, baadhi ya taasisi hizo zilifanyiwa ukaguzi maalum kufuatia ulipaji wa kima kipya cha chini cha mshahara cha Shilingi laki tatu (TZS 300,000/=) kwa sekta binafsi nchini na kubainika Taasisi 110 zinaendelea kulipa kima kipya cha chini cha mshahara kilichotangazwa na Taasisi 35 bado hazijatii Sheria hiyo. Hivyo, Kamisheni ya Kazi imewataka Waajiri kufuata Sheria za Kazi ipasavyo na kutotafuta visingizio vyoyote vya kukwepa kulipa kima hicho cha mshahara.

**59. Mheshimiwa Spika;** Pia, imethibitisha Mikataba ya kazi 1,424 (Unguja 1,112 na Pemba 312) kwa wafanyakazi ili kuhakikisha inaendana na Sheria za Kazi ikiwa ni miongoni mwa haki yao ya msingi ya wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria hizo. Wakati wa uthibitishwaji wa mikataba hiyo wafanyakazi husika husomewa mikataba yao na Maafisa Kazi ili kupata uelewa mzuri juu ya haki zao.

**60. Mheshimiwa Spika;** Kupitia kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi imepokea migogoro ya kazi 105 iliyowasilishwa (Unguja 103 na Pemba 2). Kati ya hiyo, Migogoro Ishirini na Tano (25) ni ya kuvunjika kwa Ajira, mgogoro mmoja (1) madai ya Mshahara,

migogoro 25 inaendelea ipo katika hatua ya usuluhishi na Migogoro hamsini na nne (54) imesuluhishwa tayari. Migogoro hiyo inahusu kukatishwa Mikataba ya Kazi kwa wafanyakazi, kutokulipwa kwa kiwango cha Mshahara stahiki kwa mujibu wa Sheria na kufukuzwa kazi.

**61. Mheshimiwa Spika;** Kamisheni ya Kazi imewapatia Vibali vya Kazi jumla ya Wafanyakazi wa kigeni 1,129 kutoka Nchi za Italy, India, China, Uingereza na Afrika ya Mashariki kufanya kazi nchini. Idadi kubwa ya wafanyakazi waliopatiwa vibali hivyo ni kutoka Sekta Binafsi (hoteli na Vyuu) na Sekta za Umma (Afya, Ujenzi na Utalii).

**62. Mheshimiwa Spika;** Afisi ya Mrajis imefanya ukaguzi katika Vyama vinane (8) ambavyo ni ZASU, ZUPHE, CHODAWU-Z, TUICO-Z, ZAFICOWU, ZAMAWU, ZANEMA, TEWUTA-Z na kubaini kuwa Vyama vyote hivyo vinafanya kazi zake kulingana na Katiba za Vyama vyao zinavyoelekeza ikiwemo kufanya vikao vya chama kikatiba, kuhifadhi kumbukumbu za chama na kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Mrajis wa Vyama vya Wafanyakazi. Pia, imepitia na kusajili marekebisho ya Katiba za Vyama vya wafanyakazi vya ZUPHE, ZAPSWU, na ZATUC.

**63. Mheshimiwa Spika;** Programu imetoa elimu ya Sheria za Kazi kwa Taasisi 6 Uguja na Pemba na imerusha hewani vipindi kumi na saba (17) kuhusiana na elimu ya Sheria za Kazi kupitia vyombo mbali mbali vya habari vikiwemo; ZBC TV, ZBC Redio, Chuchu FM, Island TV, Alfalah TV, ZCTV, Alsalam TV, Alfatah TV. Lengo la taaluma hiyo ni kujenga uelewa kwa waajiri, wafanyakazi na jamii kwa ujumla juu ya Sheria za Kazi. Pia, imetoa elimu kuhusiana na maswala ya Ajira za Watoto kupitia Hits FM redio na kufafanua Sheria zinazowalinda Watoto Pamoja na adhabu zake kwa Watoto ambao wanahusishwa katika maswala ya kazi chini ya umri wa miaka kumi na nane (18).

**64. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamisheni ya Kazi kupitia programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimataifa na Majadiliano ya Pamoja mbali na majukumu mengine Itafanya ukaguzi kazi kwa Taasisi 600; Itathibitisha Mikataba ya Kazi kwa wazalendo 5,000; Itakagua Vyama vya Waajiri na Wafanyakazi 15;

itatoa elimu ya Sheria za Kazi kwa Taasisi 40 na itarusha vipindi 25 kupitia vyombo vya habari.

**65. Mheshimiwa Spika,** Ili Programu ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimatifa na Majadiliano ya Pamoja iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022; naliomba Baraza lako kuidhinisha Ruzuku ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Tisini na Sita, Laki Tisa** (Tshs.1,496,900,000) kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

### **3.2.3 PROGRAMU KUU PA0703: UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

#### **3.2.3.1 Programu ndogo SA070301: Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.**

**Lengo Kuu:** Kuimarisha upatikanaji wa Mikopo nafuu kwa Wananchi.

**66. Mheshimiwa Spika;** Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umeanzishwa kwa madhumuni ya kuwawezesha wananchi wenye kipato kidogo kupata mitaji ya kufanya shughuli za uzalishaji ili kujiajiri na kuinua vipato vyao. Walengwa wakuu wa Mfuko ni Vijana, Wanawake, Wanafunzi waliomaliza elimu ya Vyuvo vikuu, Vyuvo vya Amali na Sekondari, Wastaafu na Watu walio katika makundi maalum.

**67. Mheshimiwa Spika;** Mfuko umetoa mikopo 617 Unguja na Pemba. Mikopo ya vikundi ni 156 na ya mtu mmoja mmoja ni 461. Kati ya vikundi 156, vikundi 35 ni vya makundi maalum ya Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu na vikundi vilivyobaki 121 ni mchanganyiko wa makundi hayo. Mikopo iliyotolewa ina thamani ya **Shilingi Milioni Mia Sita Thelasini na Saba, Laki Nne Ishirini na Tano Eflu** (Tshs. 637,425,000) ambapo Pemba zimetolewa **Shilingi Milioni Mia Mbili na Ishirini na Moja na Laki Tisa** (Tshs.221,900,000) na Unguja zimepewa **Shilingi Milioni Mia Nne na Tano, Laki Tano na Eflu Ishirini na Tano** (Tshs.405,525,000) kama inavyoonekana katika Kimbatanisho nambari 4 na 5 kinahusika.

**68. Mheshimiwa Spika;** Katika mikopo 617 iliyotolewa, mikopo 264 ni ya Mradi wa kilimo cha Matunda na Mboga mboga. Mradi huu peke yake umetoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi Milioni Mia Mbili na Sabini na Nne, Laki Tatu Arubaini Eflu** (Tsh. 274,340,000). Mikopo mingine 353 yenye thamani ya **Shilingi Milioni Mia Tatu Sitini na Tatu, Thamanini na Nne Eflu, Mia Sita Arobaini na Saba** (Tsh. 363,084,647) imetolewa kwa kuendesha shughuli za kiuchumi kama vile biashara za jumla na rejareja, utoaji huduma za kutuma na kupokea fedha, uuzaji wa vinywaji baridi, uvuvi, viwanda vidogo vidogo, ufugaji wa mbuzi, kuku, ng'ombe, uchongaji na kazi za mikono.

**69. Mheshimiwa Spika;** Mfuko umefanikiwa kuongeza uwezo wa kukopesha baada ya kupata Mradi wa pili wa uendelezaji kilimo cha Mboga na Matunda wenye thamani ya **Shilingi Milioni Mia Moja** (Tshs.100,000,000) kutoka Mradi wa FEED THE FUTURE ikiwa ni sehemu ya mikakati ya Mfuko kutunisha fedha zake. Mradi wa kwanza ulimalizika Disemba, 2020 na ulikuwa na thamani ya **Shilingi Milioni Mia Tatu na Hamsini** (Tsh. 350,000,000).

**70. Mheshimiwa Spika;** Mikakati mingine ambayo imeuwezesha Mfuko kupata fedha za ziada, ni uwekezaji wa sehemu ya fedha zake katika Benki ya Biashara PBZ Ltd ambapo Mfuko ulipata faida ya **Shilingi Milioni Arobaini** (Tsh. 40,000,000) baada ya kuwekeza **Shilingi Milioni Mia Tano** (Tsh. 500,000,000) na mkakati wa tatu ni kutoa mikopo midogo midogo na ya muda mfupi wa miezi sita hadi tisa. Hivyo, kuwezesha kutoa mikopo mingi kwa muda mfupi kutokana na kasi ya mzunguko wa fedha za mikopo.

**71. Mheshimiwa Spika;** Jumla ya **Shilingi Milioni Mia Tatu na Tisa, Laki Tisa Hamsini Eflu na Mia Saba** (Tshs. 309,950,700) zimekusanywa Unguja na Pemba katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai, 2020 hadi Machi, 2021. Pemba zimekusanya **Shilingi Milioni Mia Moja na Mbili, Laki Sita Thalathini na Tano Eflu na Mia Mbili** (Tshs. 102,635,200) na Unguja imekusanya **Shilingi Milioni Mia Mbili na Saba, Laki Tatu Kumi na Tano Eflu** (Tshs. 207,315,000).

Marejesho haya ni wastani wa **Shilingi Milioni Thalathini na Nne, Laki Nne Thalathini na Nane Eflu, Mia Tisa Sitini na Saba** (Tshs. 34,438,967) kila mwezi, wakati Mfuko umejipangia kukusanya **Shilingi Milioni Arobaini** (Tshs. 40,000,000) kwa mwezi Kiambatanisho Nambari 6 kinahusika.

**72. Mheshimiwa Spika;** Katika kuleta ufanisi wa biashara za wajasiriamali wanaopewa mikopo, Mfuko unahakikisha unawajengea uwezo wakopaji wote kwa nia ya kujifunza kwa vitendo na kwa nadharia. Pia, Mfuko uliwawezesha wakulima 52 (wanawake 32 na wanaume 20) wa Wilaya nne (4) za Pemba kufanya ziara ya Mafunzo katika kijiji cha Pujini kilichoko katika Wilaya ya Chake Chake Mkoa wa Kusini Pemba kwa lengo la kujifunza ukulima wa tungule na mchicha kutoka kwa wakulima wa Pujini. Wanafunzi hao walijifunza ukulima wa mazao hayo kwa kutumia mbolea za asili bila ya kutumia kemikali ambapo walijionea maendeleo na uzalishaji mkubwa wa mazao hayo.

**73. Mheshimiwa Spika;** Mfuko uliandaa ziara maalum katika vijiji vya Ungi, Tumbe, na Msuka kwa Pemba na Uroa, Chwaka na Marumbi kwa Unguja katika jitihada za kufufua zao la Mwani katika maeneo hayo ili kwenda sambamba na kuzitumia kwa ukamilifu rasilimali za baharini. Wajasiriamali waliotembelewa katika maeneo hayo ni wale waliopatiwa boti na Mfuko. Wakulima hao wamelalamikia bei ndogo ya bidhaa hiyo na tatizo la soko kwa ujumla. Pia, Mfuko umetoa mafunzo kwa wajasiriamali 1,082 (Unguja 554 na Pemba 528) kati ya hao, Wanawake 565 na Wanaume 517 kutoka katika Wilaya zote 11 za Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalihusu kilimo bora, ubunifu wa miradi yenye tija, masuala ya usimamizi wa Fedha, kuongeza thamani na Masoko ya bidhaa na mazao ya wakulima na wajasiriamali wengine.

**74. Mheshimiwa Spika;** Katika kudhibiti upoteaji wa fedha za Serikali, Mfuko wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi umefanikiwa kukusanya fedha za marejesho ya mikopo kwa njia ya elektroniki. Utaratibu ambao umeanza kisiwani Pemba na utawezesha kuhakikisha usalama wa fedha na kupunguza gharama za ufuatiliaji.

**75. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umejipangia Kutoa mikopo 770 yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Nane (TSh. 800,000,000/=) kwa vikundi vya kiuchumi na mjasiriamali mmoja mmoja katika sekta zote za kiuchumi; itasimamia urejeshaji wa mikopo; itafanya ufuatiliaji; itaimarisha uwekaji wa kumbukumbu za wateja wa mikopo; itaendelea kutunisha fedha za Mfuko; itaimarisha mashirikiano na uratibu na taasisi zinazotoa mikopo nafuu; itajenga uwezo wa watendaji ili kuongeza ufanisi wa kazi; itafanya mapitio ya Muongozo wa Usimamizi wa Mikopo; itaratibu uandaaji wa Sheria ya Uendeshaji wa Mfuko; itashirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda (Kupitia SMIDA) na Benki ya Watu wa Zanzibar - PBZ Ltd kufanikisha uendeshaji wa Mpango wa Maendeleo ya Wajasiriamali Wadogo Wadogo na wa Kati unaopata ufadhili wa Mfuko wa Khalifa.

**76. Mheshimiwa Spika;** ili Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi uweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako liidhinishe Ruzuku ya **Shilingi Milioni Mia Tatu Kumi na Nane, Laki Mbili na Elfu Saba** (Tshs. 318,207,000) kwa ajili ya kazi za kawaida.

### **3.2.3.2 Programu Ndogo: SA070302: Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika.**

**Lengo kuu:** Kusimamia mageuzi ya Mfumo wa Ushirika ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika kuchangia katika kukuza ajira na uchumi wa Nchi

**77. Mheshimiwa Spika;** Programu hii ina lengo la kusimamia Mageuzi ya Mfumo wa Vyama vya Ushirika ili viwe imara, endelevu, vinavyoendeshwa kiujasiriamali na vinavyokidhi mahitaji ya wanachama, kiuchumi na kijamii. Pia, inachangia kukuza ajira na pato la Taifa.

**78. Mheshimiwa Spika;** Programu imefanikiwa kusajili Vyama vya Ushirika 318 (Unguja: 155; Pemba: 163), ambapo SACCOS ni moja na vyama vya uzalishaji 317 zoezi hili limeongeza idadi ya Vyama vilivyosajiliwa kufikia 4,877. Pia, imevijengeza uwezo Vyama vya Ushirika kwa kutoa mafunzo elekezi juu ya uandaaji wa Mpango Biashara,

Uandishi wa vitabu vya hesabu, marekebisho ya katiba, elimu ya fedha na Mbinu za kuongeza Mitaji kwa washiriki 1,638 (Wanaume 592 na Wanawake 1,046) kwa viongozi na wanachama. Mafunzo hayo elekezi yalitolewa kwa vyama 375 (SACCOS 38 na Vyama vya Uzalishaji 337).

**79. Mheshimiwa Spika;** Programu imesimamia Mabaraza ya Ushirika Kiwilaya ambapo wanachama 441 (wanawake 175 na wanaume 266) kutoka kwenye vyama 106 (SACCOS 86 na Uzalishaji 20) walifikiwa. Lengo ni kuwapa fursa ya kujadili mafanikio na changamoto zinazovikabili vyama vyao. Changamoto kubwa ni kutokufuatwa maelekezo ya kisheria katika utekelezaji wa shughuli zao. Aidha, dhana mpya ya Uchumi wa buluu ilitolewa kwa lengo la kuimarisha ushirika wao katika eneo hilo.

**80. Mheshimiwa Spika;** Programu imefuatilia na kuvifanyia uchunguzi Vyama 266 (119 Pemba na Unguja 147) ambapo matokeo yameonesha kuwa vyama vya uzalishaji vina mitaji midogo, utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa elimu kwa viongozi na wanachama unahitaji kuendelezwa. Kwa upande wa SACCOS hali ya ukuaji wa mitaji inazidi kuimarika kufikia **Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Mia Nne Sabiini** (Tshs. 17,470,000,000). Unguja ni **Shilingi Bilioni Kumi na Nne, Milioni Mia Moja na Thamanini** (Tshs. 14,180,000,000) na Pemba ni **Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Mbili Tisini** (Tshs. 3,290,000,000). Pia, imekagua Vyama 144 (Pemba 57 na Unguja 87). Matokeo yameonesha changamoto za mitaji midogo, utunzaji wa kumbukumbu hasa za hesabu na masuala ya utawala bora katika uendeshaji wa vyama unahitaji kuimarishwa, Afisi inazifanyia kazi changamoto hizi kwa kutoa mafunzo ya vitendo na ukaguzi wa mara kwa mara.

**81. Mheshimiwa Spika;** Programu imeadhimisha Siku ya Ushirika Duniani iliyofanyika tarehe 4/7/2020 ambapo wanaushirika walipata fursa ya kuzungumza na kuutangaza ushirika kupitia vyombo mbali mbali vya habari na kushiriki katika upandaji wa mikoko kwa lengo la kuhifadhi mazingira, kauli mbiu ya Ushirika ni **"Ushirika na Mabadiliko ya Tabia Nchi."** Vile vile, katika kuimarisha mashirikiano kati ya vyama vya ushirika vya Zanzibar na Tanzania Bara, Programu

imesimamia ziara nne za mafunzo zilizoandaliwa na Vyama vya Ushirika. Aidha, SACCOS mbili kutoka Tanzania Bara (Elimu SACCOS na NOSACCU) zilitembelea Zanzibar na SACCOS mbili za Zanzibar (Raudha Multipurpose na Makuli multipurpose) zilitembelea Tanzania Bara. Ziara zimesaidia kuelimisha vyama kujikita katika uzalishaji wenye tija na kuimarisha mashirikiano kupitia mnyororo wa thamani.

**82. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Programu ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika imepanga kusajili Vyama vya Ushirika 400; Kukagua mahesabu ya vyama 350; Kufanya ukaguzi wa kawaida na kutoa miongozo kwa vyama 1,000; Kujenga uwezo wa kiutendaji wa vyama vya ushirika 950 na kuwajengea uwezo viongozi 685 wa SACCOS.

**83. Mheshimiwa Spika,** Ili Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba baraza lako kuidhinisha jumla ya **Shilingi Milioni Mia Sita Sitini na Sita, Laki Saba na Hamsini Eflu** (Tsh.666,750,000) kwa ajili ya kazi za kawaida.

### **3.2.3.3 Programu Ndogo SA070303: Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.**

**Lengo Kuu:** Kukuza Hadhi ya kiuchumi kwa Vijana, Wanawake, Watoto, Watu wazima na Makundi maalum katika jamii.

**84. Mheshimiwa Spika;** Programu hii inasimamiwa na Idara ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na ina jukumu la kubuni na kuratibu programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuwawezesha vijana kujiajiri na kuwa na kipato endelevu cha kuweza kumudu maisha yao. Pia, Programu inasimamia uendeshaji wa vituo viwili ambavyo vinasaidia utekelezaji wa shughuli za ujasiriamali navyo ni: Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali kilichopo Mbweni na Kituo cha Wanawake cha kutengeneza vifaa vya umeme wa jua kilichopo Kinyasini.

**85. Mheshimiwa Spika;** Katika kukuza ujasiriamali nchini, Programu imeendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wajasiriamali kutoka katika Wilaya za Unguja na Pemba. Jumla ya Wajasiriamali 175 (170 wanawake na 5 wanaume) kutoka katika kaya masikini Unguja na wajasiriamali 129 (100 wanawake na 29 wanaume) Pemba wameshiriki katika mafunzo hayo. Vile vile, imevitembelea vikundi vya wajasiriamali 91 (50 Unguja na 41 Pemba) na kuvipatia ushauri stahiki wa kuboresha vikundi vyao na shughuli za ujasiriamali wanazozifanya katika vikundi hivyo. Pia, imeendelea kutoa ushauri wa kibiashara kwa wajasiriamali wa Unguja ambapo jumla ya wajasiriamali 114 wamepatiwa ushauri huo.

**86. Mheshimiwa Spika;** Programu ilifanya Mkutano wa wajasiriamali kutoka katika Wilaya za Unguja pamoja na Maafisa wanaoshughulika na wajasiriamali ili kujadiliana juu ya masuala ya kuimarisha ujasiriamali pamoja na kubaini changamoto za wajasiriamali ili kuweza kuzipatia ufumbuzi wake. Jumla ya wajasiriamali 40 (12 wanaume na 28 wanawake) na maafisa 19 walishiriki katika Mkutano huo. Miongoni mwa changamoto zilizobainika ni pamoja na uhaba wa mafunzo ya kuimarisha uzalishaji, vifaa na mitaji ya kuimarisha biashara zao. Mikutano hii inawasaidia watendaji kubuni mipango bora ya kuwasaidia wajasiriamali nchini.

**87. Mheshimiwa Spika;** Aidha, Afisi imesimamia uendeshaji wa Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali (ZTBI) ambapo mafunzo ya ujasiriamali na usarifu wa maziwa na matunda yametolewa kwa wajasiriamali 181. Kufuatia mafunzo hayo jumla ya kampuni ndogo ndogo 15 zimeundwa na kusajiliwa. Vile vile, imesimamia uendeshaji wa Kituo cha Wanawake cha Utengenezaji wa Vifaa vya Umeme wa Jua (Barefoot college) kilichopo Kibokwa Kaskazini Unguja ambapo jumla ya Wanafunzi 12, (4 Unguja na 8 Pemba) wamefundishwa kutengeneza vifaa vya umeme wa jua, wanafunzi 7 mafunzo ya kushona nguo za nyuki na za kawaida na wanafunzi 15 wamemaliza mafunzo ya ufugaji wa nyuki na kupatiwa mizinga 30 pamoja na vifaa vyote vya kuanzia mradi wa nyuki. Aidha, Kituo kimetoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana wanawake 80 kwa kushirikiana na Youth Challenge International.

**88. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu ya Uratibu na Uendelezaji wa Program za Wananchi Kiuchumi imepanga kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa Vijana 250; itaendelea kuimarisha huduma za ushauri wa kibiashara kwa wajasiriamali wa Wilaya (EBDS) wakiwemo Wanawake na Makundi maalum; itaandaa miradi 3 ya kuwawezesha wajasiriamali na vijana kutoa huduma na bidhaa zenye ubora; Itawawezesha wajasiriamali 28 kushiriki katika maonesho ya Afrika Mashariki (Jua Kali); Itaendelea kuwawezesha vijana 210 kujijari kupitia Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali pamoja na Kuwawezesha Kiuchumi Wanawake 80 (25 umeme wa jua na 55 kujikimu kimaisha) kupitia kituo cha Wanawake cha Utengenezaji wa Vifaa vya Umeme wa jua Kibokwa.

**89. Mheshimiwa Spika;** ili program ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Program za Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Sita Arobaini na Tisa, Laki Nane Hamsini na Tisa Elfu** (Tshs.6,649,859,000) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

### **3.2.4 PROGRAMU KUU PA0704: KUIMARISHA UWEKEZAJI NA SHUGHULI ZA SERIKALI KIKANDA NA KIMATAIFA**

**Matokeo ya muda mrefu:** Kuimarika kwa Mashirikiano na Uwekezaji wenye tija kwa maendeleo ya nchi na ustawi wa wananchi.

#### **3.2.4.1 Programu ndogo SA070401: Maendeleo ya Ukuwaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji.**

**Lengo Kuu:** Kuwezesha Mitaji Binafsi Kuwekezwa Nchini.

**90. Mheshimiwa Spika;** Programu ya Maendeleo ya Ukuwaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji inatekelezwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar na inalengo la kuweka mazingira mazuri ya kisera, kisheria na uimarishaji wa huduma mbali mbali zitakazo imarisha uwekezaji nchini.

**91. Mheshimiwa Spika;** Programu inaendelea kufanya ushajiishaji wa fursa za uwekezaji uliolenga zaidi katika sekta ya viwanda na bahari kuu kwa njia ya mtandao katika nchi ya Malaysia, Philippine, Singapore, Indonesia, Sweden, Afrika Kusini, Abudhabi, Harare na Dubai. Afisi kupitia ZIPA ilipokea miradi 35 inayokusudia kukezwa ya Sekta mbali mbali na kuyafanyia upembuzi ambapo miradi 30 ilipatiwa vibali vya uwekezaji yenye mtaji wa makisio ya Dola za Kimarekani **Milioni Moja na Sabiini na Mbili, Laki Moja Ishirini na Nane na Mia Nane** (\$172,128,800) imeidhinishwa na kuingizwa katika Database ya Mamlaka katika kipindi cha Julai 2020 hadi Machi 2021. Miradi hiyo iliyoidhinishwa inatarajiwa kuzalisha ajira zisizopungua 1,886 kwa wenyeji.

**92. Mheshimiwa Spika;** Programu inaendelea kufanya Utafiti wa Mitaji Binafsi (Private Capital Flow) kwa kushirikiana na Bank Kuu ya Tanzania tawi la Zanzibar pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Utafiti huo upo katika mzunguko wa 12 na uko katika hatua za uchambuzi wa data na uandishi wa ripoti. Utafiti huu unafanywa ili kujua muelekeo na maendeleo ya uwekezaji wa mitaji binafsi nchini na changamoto zake ili kuishauri Serikali juu ya uwekezaji. Vile vile, unasaidia kuelewa masuala ya urari wa biashara, ripoti hii ni sehemu ya ripoti ya uwekezaji ya dunia (World Investment Report).

**93. Mheshimiwa Spika;** Katika kuhakikisha kuwa miradi inaendesha shughuli zake kwa kufuata masharti na utaratibu unaotakiwa katika Maeneo Huru ya Uchumi, Afisi imekarabati mabanda matatu; inaendelea na usimamizi wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi Fumba; imeandaa mpango wa gharama (BoQ) za ukarabati wa mitaro ya maji machafu, ujenzi wa ukuta unaozunguka Mtaa wa Viwanda Amani na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya maeneo huru Micheweni yamekamilika. Aidha, Mamlaka imelipa fidia kwa Wananchi wa Micheweni ambao wamepisha ujenzi wa barabara inayokwenda katika Maeneo Huru ya Uchumi Micheweni.

**94. Mheshimiwa Spika;** Afisi ilifanya ziara 26 katika maeneo ya miradi ya sekta mbali mbali za uwekezaji kuangalia maeneo mapya yanayotaka kukezwa. Pia, jumla ya miradi 14 ilifanyiwa ukaguzi kuangalia maendeleo yake na maombi 429 ya vibali vya kazi na ukaazi yamepokelewa. Kati ya hayo 189 ni maombi mapya, 150 kuongeza muda wa vibali vya kazi, 38 kuongeza muda wa vibali vya ukaazi na vibali 55 vilifutwa kwa sababu mbali mbali.

**95. Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa wawekezaji, ZIPA inaendelea kuimarisha Kituo cha Huduma Jumuishi kwa Wawekezaji "One Stop Centre" ambacho kinatoa huduma zikiwemo vibali vya kazi na ukaazi, vibali vya ujenzi, usajili wa makampuni na huduma za kodi na mazingira kwa wawekezaji. Kitengo kina maafisa waandamizi kutoka katika taasisi 8 muhimu zinazotoa huduma kwa wawekezaji ambazo ni ZEMA; Kamisheni ya Ardhi, BPR, Uhamiaji, Kamisheni ya Kazi, Bodi ya Mapato (ZRB), Mamlaka ya Mapato Tanzania, DCU. Watendaji wa 'One Stop Center' wanaendelea kutoa huduma zao kwa ufanisi na utoaji wa vibali umepungua kutoka wiki tatu hadi wiki moja.

**96. Mheshimiwa Spika;** katika kutatua changamoto ya upatikanaji wa ardhi kwa uwekezaji nchini, ZIPA inaendelea na zoezi la kufanya utafiti wa kuyatambua maeneo ya Ardhi ya Akiba (Land Bank) kwa uwekezaji nchini. Kikosi kazi (Task force) kilichojumuisha Kamisheni ya Ardhi, ZIPA, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Masheha kimeundwa na tayari kazi ya kuyatambua maeneo na kuyaweka katika ramani imeshafanywa na imehusisha Mikoa mitano ya Zanzibar ambayo imegawiwa kwa mfumo wa zoni 5. Utaalamu wa kisasa kwa kutumia ndege zisizo na rubani (drones) umetumika kupata taarifa za yaliyomo ndani ya maeneo hayo. Hivi sasa kazi ya kuandaa ripoti ya awali itakayowasilishwa Serikalini imekamilika na tayari imeshwasilishwa kwa baadhi ya wadau ili kutoa michango yao. Ardhi hiyo ya Akiba itatumika kwa uwekezaji wa aina mbali ikiwemo kilimo, mafuta, gesi na uchumi bluu.

**97. Mheshimiwa Spika;** Afisi kupitia ZIPA imekamilisha Mpango Mkuu wa Matumizi ya ardhi katika Maeneo Huru ya Uchumi Micheweni na matayarisho ya kupeleka Miundo mbinu ya msingi kama vile Barabara, Umeme na Maji zinaendelea. Ni matumaini yetu kuwa maeneo haya sasa yataweza kuvutia wawekezaji wengi kwa manufaa ya nchi na jamii iliyoizunguka.

**98. Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo ya Maendeleo ya Ukuwaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2021/2022 itatangaza na kushajiisha uwekezaji katika sekta za uvuvi, ufugaji wa mazao baharini, uvuvi wa bahari kuu na utalii wa hadhi ya juu; itaendeleza miundombinu ya barabara, maji, umeme na huduma nyengine itakayopelekea kurahisisha uwekezaji katika Maeneo Huru ya Uchumi; itashajiisha uwekezaji katika kuanzisha miji ya kibiashara; itashajiisha wawekezaji kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu ikiwemo gati za uvuvi, vyumba baridi vya kuhifadhi samaki na mazao mengine ya bahari, viwanda vya kusarifu na kusindika samaki.

**99. Mheshimiwa Spika;** Pia, Programu itaandaa Mpango Mkuu wa Uwekezaji na uwekaji wa miundo mbinu katika Mtaa wa viwanda (Industrial park); itaendeleza usimamizi wa uwekaji wa miundombinu katika Maeneo Huru ya Uchumi Fumba, Micheweni na Mtaa wa Viwanda Amani na itavutia wawekezaji kuwekeza katika viwanda vya kusarifu mazao ya kilimo, uvuvi, vifaa vya maziwa, viwanda vya vifungashio na viwanda vya madawa; itashajiisha wawekezaji kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji maji na "green houses" kwa ajili ya kuzalisha pamoja na mazao mengine, mboga mboga, matunda, viungo, mazao asili pamoja na uwekezaji wa mifugo na kuunganisha uzalishaji huu kwa kuongeza thamani.

**100. Mheshimiwa Spika;** ili Programu ndogo ya Maendeleo ya Ukuwaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako liidhinisha Ruzuku na Fedha za Maendeleo jumla ya **Shilingi Bilioni**

**Nane, Milioni Mia Mbili Hamsini na Nane, Laki Tano**  
(Tshs.8,258,500,000).

### **3.2.4.2 Programu Ndogo SA070402: Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

**Lengo Kuu:** Kukuza, kuratibu na kuimarisha Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika sekta za kiuchumi na kijamii pamoja na kutekeleza miradi mbali mbali ya Maendeleo.

**101. Mheshimiwa Spika;** Programu imefanya Marekebisho ya Sheria Namb. 8 ya mwaka 2015 ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kutoa fursa zaidi za kuvutia wawekezaji kutoka katika sekta ya Umma kushirikiana na Sekta binafsi kwa lengo la kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Marekebisho ya Sheria yalikusisha maoni ya wadau wakiwemo Wawekezaji, Kamati ya Makatibu Wakuu, Baraza la Mapinduzi, Kamati ya Sheria ya Baraza la Wawakilishi na hatimae kuidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

**102. Mheshimiwa Spika;** Katika kuimarisha uwekezaji kupitia PPP, Programu imekamilisha upitiaji wa nyaraka za zabuni kwa miradi 13 ya awali ya PPP kwa hatua za kuitangaza ili kupata mwekezaji ambaye atawekeza katika miradi hiyo. Nyaraka za zabuni (Request for Qualification, Request for Proposal na PPP Agreement) zimewasilishwa kwa 'Implementing Authority' kwa hatua za kutangaza zabuni.

**103. Mheshimiwa Spika;** Aidha, Programu imepokea maombi 35 ya wawekezaji walioonyesha dhamira ya kufanya uwekezaji nchini katika maeneo mbali mbali Zanzibar. Kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi husika za Serikali, Afisi inaendelea na mazungumzo kwa hatua ya kusaini makubaliano kwa wawekezaji 6 ambao wanakamilisha taratibu za uwekezaji kwa miradi ya PPP. Miradi hiyo ni pamoja na miradi ya Uvuvi, Kituo cha Maonyesho ya Biashara na Mikutano, Ujenzi wa Uwanja wa ndege Pemba, kuliendeleza eneo la hoteli ya Bwawani na "Zanzibar Tower (Domino)."

**104. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Programu ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi itapitia na kuidhinisha miradi mikubwa na midogo iliyowasilishwa Idara ya PPP; itaratibu uchambuzi wa kisheria, mazingira na kijamii kwa Miradi ya PPP; itajenga uwezo juu ya Usimamizi wa Mikataba ya Miradi ya PPP; itatayarisha na kupitia nyaraka za zabuni za miradi; itaanzisha mfumo wa kuratibu malalamiko kwa waathirika wa mradi; itandaa Kanuni na Mwongozo wa miradi inayoasisiwa na Mwekezaji Binafsi (unsolicited proposal); itandaa modeli za kifedha na uchambuzi wake kwa miradi ya PPP; itajenga uwezo kwa Kamati ya wataalamu na Taasisi za Serikali na sekta binafsi juu ya dhana ya PPP na miundo ya Kimazingira na kijamii; itachapisha na kutafsiri nyaraka za PPP (Sera, Sheria na Miongozo); itahudhuria mikutano inayohusiana na masuala ya uwekezaji kwa njia ya PPP ndani na nje ya nchi na itaratibu kufanya upembuzi yakinifu kwa miradi mipya yenye tija ya PPP.

**105. Mheshimiwa Spika;** ili Program ndogo ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako kuizinisha jumla ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Kumi na Sita, Laki Moja Hamsini Eflu** (Tshs.1,516,150,000) kwa kazi za kawaida na maendeleo.

### **3.2.4.3 Programu ndogo SA070403: Uratibu wa Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi.**

**Lengo Kuu:** Kuimarisha Mtangamano wa Kikanda, Taasisi za Kimataifa na Ushirikiano mwema wa nchi marafiki.

**106. Mheshimiwa Spika;** utekelezaji wa Programu hii umeimarisha ushiriki wenye manufaa wa Zanzibar katika Jumuiya za Mtangamano wa Kikanda za SADC, EAC, IORA, Jumuiya ya Utatu (SADC – EAC – COMESA) na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) na mahusiano mazuri kati yake na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi. Kwa kutambua umuhimu wa mchango wa Wanadiaspora katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, Serikali imeendelea kuwatambua, kuwaunganisha, kuwashajihisha na kuwashirikisha Wanadiaspora wa Zanzibar katika

umoja wao ili waweze kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya Zanzibar.

**107. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeratibu ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya maandalizi ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimekuwa na mashirikiano mazuri katika kuratibu na kushiriki katika shughuli za majukwaa ya kimataifa na kidiplomasia ikiwemo kufanya mikutano ya mashauriano ya ndani kwa lengo la kupata msimamo wa pamoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hujumuisha maslahi ya Zanzibar kabla ya kuhudhuria mkutano husika.

**108. Mheshimiwa Spika,** Pia, Afisi imeshiriki katika Mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa kuondoleana vikwazo vya Biashara visivyokuwa vya kiushuru (NTB's) vilivyofanyika mjini Dodoma, Dar es Salaam na Arusha. Katika vikao hivi kumekuwa na utaratibu wa kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili wafanyabiashara katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miongoni mwa maeneo muhimu yaliojadiliwa katika mikutano hiyo ni Ibara zinazokwamisha utekelezaji wa Sheria ya kuondoa Vikwazo vya Biashara visivyokuwa vya kiushuru ya 2017.

**109. Mheshimiwa Spika;** Afisi imetoa mafunzo kwa wafanyabiashara wa Zanzibar kwa ajili ya kuwajengea uwelewa juu ya Vikwazo vya Biashara visivyokuwa vya kiushuru mwezi Oktoba, 2020 Unguja na Pemba. Mafunzo yalijikita katika kutoa muongozo juu ya changamoto, aina ya vikwazo visivyokuwa vya kiushuru, pamoja na kuzitambulisha Taasisi zenye mamlaka ya kupokea na kuratibu changamoto kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi ili Jumuiya ya Afrika Mashariki kufikia mazingira mazuri ya maendeleo endelevu ya biashara na viwanda.

**110. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeshiriki katika Mkutano wa uandaaji wa maoni ya Rasimu ya Ada na Tozo zinazotolewa na Taasisi mbali mbali za nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ilithibiti kuwepo kwa muingiliano wa tozo na ada zinazofanana zinazotozwa kupata huduma mbali mbali kwa wafanyabiashara, wawekezaji na watoa

huduma wengine ikiwemo mtumiaji wa mwisho. Mkutano uliagiza taasisi za nchi husika ziangalie uwezekano wa kupunguza au kuchanganya tozo hizo ili kuondokana na changamoto hizo.

**111. Mheshimiwa Spika;** Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ilifanya Mkutano wa 21 wa Kilele wa Wakuu wa Nchi na Serikali tarehe 27 Februari, 2021 kwa njia ya mtandao. Mkutano huo ulimteuwa Mheshimiwa Uhuru Kenyatta, Rais wa Jamhuri ya Kenya kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya EAC na nchi ya Burundi kuteuliwa kuwa Katibu wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Aidha, Mkutano huo ulimteuwa Mheshimiwa Dk. Peter Mathuki kutoka Jamhuri ya Kenya kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya EAC kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia Aprili, 2021.

**112. Mheshimiwa Spika;** Jumuiya ya Afrika Mashariki imeridhia lugha ya Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa kuwa lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kutumika katika shughuli za Jumuiya hiyo. Vile vile, Mkutano wa Kilele umejadili taarifa ya maombi ya nchi ya Somalia ya kujiunga na Jumuiya ya EAC na kuagiza kuwa mchakato wake uharakishwe. Aidha, maombi ya nchi ya DRC Congo ya kujiunga na Jumuiya ya EAC yamepokelewa na kuagiza kuharakisha kuunda Kamati ya kufanya uchunguzi (Verification Committee) wa nchi hiyo wa kujiunga na EAC kutokana na vigezo vya Jumuiya hiyo.

**113. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeratibu na kushiriki mikutano ya Umoja wa Afrika (AU) katika kuanzishwa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) ambalo limejumuisha maeneo makuu matano ya mashirikiano. Maeneo yenyewe yanajumuisha Biashara ya bidhaa, huduma, Uwekezaji, Hakimiliki (Intellectual Property Rights) na Sera za Ushindani huru (Competition Policy). Pia, Afisi imeshiriki Mkutano uolijadili Rasimu ya Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya SADC.

**114. Mheshimiwa Spika;** hatua inayoendelea baada ya kuanza utekelezaji wa Itifaki ya Biashara ya Huduma ni kutayarisha Mpango maalum wa kupata rasilimali fedha na kiufundi (AfCFTA adjustment

facility) kwa ajili ya kupunguza athari za kupotea mapato wakati wa utekelezaji huo. Kupitia Mfuko maalum utakaoanzishwa, nchi wanachama na taasisi binafsi wataweza kukopa baada ya kutimiza vigezo maalum vilivyowekwa. Majadiliano ya suala hili bado yanaendelea.

**115. Mheshimiwa Spika;** kwa upande wa shughuli zinazofanyika katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Afisi imeratibu ushiriki wa Zanzibar katika Mkutano wa Kilele wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC uliofanyika mwezi Agosti, 2020 kwa njia ya mtandao. Katika mkutano huo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikabidhi Uenyekiti wa Jumuiya ya SADC kwa nchi ya Msumbiji. Masuala mengine yaliojadiliwa katika mkutano huo ni uanzishaji wa kituo cha SADC cha Huduma za Kibinadamu na Matukio ya Dharura (SADC Humanitarian and Emergency Operations Centre) pamoja na ombi la Msumbiji la kutaka kuteuliwa kuwa Mwenyeji wa Kituo hicho muhimu katika matayarisho na kukabiliwa na maafa.

**116. Mheshimiwa Spika;** Pia, Afisi imeratibu ushiriki wa Zanzibar katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri la SADC uliofanyika tarehe 8 hadi 13 Machi, 2021 kwa njia ya mtandao. Mkutano huu ulikuwa na ajenda kuu ya kupitisha bajeti ya Jumuiya ya SADC kwa mwaka 2021/2022 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Bajeti ya mwaka 2020/21 ya Jumuiya iliidhinisha michango ya Dola za Marekani milioni 47.407 kwa Nchi Wanachama. Hadi tarehe 23 Novemba, 2020 kiasi cha Dola za Marekani milioni 35 zilipokelewa ikiwa ni sawa na asilimia 74 ya bajeti hiyo. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekamilisha mchango ulioidhinishwa kulipa kwa mwaka huo ambao ulikuwa ni Dola za Marekani Milioni 3.114.

**117. Mheshimiwa Spika;** Mkutano wa Baraza la Mawaziri la SADC umeidhinisha bajeti ya Dola za Marekani Milioni 47.407 kwa mwaka 2021/22 ikiwa ni mchango kutoka Nchi Wanachama. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepangiwa kutoa mchango wa Dola za Marekani milioni 3.330 katika bajeti hiyo. Aidha, katika Mkutano huo wa Mawaziri, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa na ombi maalum la mazingatio ya utekelezaji wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika

Jumuiya ya SADC. Mazingatio hayo yalilenga kuifanya lugha ya Kiswahili kuanza kutumika kuwa lugha ya kazi ya SADC katika nyaraka zote.

**118. Mheshimiwa Spika;** Aidha, Afisi imeshiriki katika mikutano ya Tume za kudumu za pamoja kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nchi za Namibia, Sychelles na Burundi. Katika mikutano hio yalijadiliwa masuala ya kuimarisha mashirikiano katika sekta za utalii, biashara, usafiri, uwekezaji, miundombinu, ulinzi na usalama mipakani na Diplomasia. Katika mashirikiano hayo, zipo fursa nyingi za kuichumi ambazo wananchi wanaweza kuzifikia ili kuongeza wigo wa mapato yao. Miongoni mwa fursa hizo ni pamoja na Zanzibar kupokea na kusafirisha watalii kupitia makampuni yao kwa watalii ambao watatembelea nchi hizo kwa wakati mmoja.

**119. Mheshimiwa Spika;** Katika muendelezo wa kuwashajihisha na kuwashirikisha Wanadiaspora kuchangia maendeleo ya Kijamii na kiuchumi ya Zanzibar, Afisi imeendelea kutoa taaluma kwa Wanadiaspora wanaofika katika Afisi zetu. Hamasa na muitikio wa wanadiaspora wetu umekuwa ukiongezeka kila siku. Pia, Afisi imekuwa ikizitafutia suluhisho changamoto za wanadiaspora mara tu zinapotufikia kwa kushirikiana na taasisi husika.

**120. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeanza kutoa elimu kuhusu Sera ya Diaspora ya Zanzibar ya mwaka 2017 na Sheria namba nne ya mwaka 2020 inayohusu mambo ya Diaspora Zanzibar kwa wanadiaspora na wananchi kwa jumla kupitia njia tofauti za mawasiliano ikiwemo Redio, Televisheni, Magazeti na Mitandao ya kijamii kama vile Instagram na Whatsapp. Vile vile, Afisi imefanikiwa kuanza shughuli za uandaaji wa kanzi data itakayofanikisha kupata taarifa sahihi za Diaspora ambazo zitatwezesha kupanga shughuli za kiseru na maendeleo baada ya kutambua idadi yao, walivyotawanyika kijiografia, jinsi, ujuzi, uzoefu, utashi wao pamoja na uwezo wa Jumuiya zao huko wanakoishi.

**121. Mheshimiwa Spika;** katika kuitikia wito wa Serikali, Wanadiaspora wanaendelea kutoa michango mbali mbali ya kijamii. Afisi imeendelea kuratibu upokeaji na ukabidhishaji wa michango hiyo ikiwemo vifaa vya msaada katika sekta ya Elimu na Afya kwa Skuli ya

Sekondari Kikungwi, Hospitali ya Wilaya ya Kaskazini "A" Kivunge na Kituo cha Afya Uzi vilivyotoka kwa Wazanzibari wanaoishi nchini Denmark (AHAS GROUP). Vile vile, Afisi inaendelea kuratibu na kufanikisha shughuli za itifaki za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa ufanisi na uweledi zaidi. Shughuli hizi zinajumuisha uwekaji wa mawe ya msingi na ufunguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo, matukio ya kijamii, mikutano, sherehe za kitaifa, ziara za ndani, uratibu na ufuatiliaji wa maombi ya viza kwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na upokeaji wa wageni wa kitaifa na kimataifa.

**122. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeratibu ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya maandalizi ya Mikutano ya kuondoleana vikwazo vya Biashara visivyokuwa vya kiushuru (NTB's), kikao cha uandaaji wa maoni juu ya Rasimu ya ada na tozo zinazotolewa na taasisi mbali mbali katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kilichofanyika Dodoma, kikao kilijadili mapendekezo na msimamo wa bidhaa za Tanzania zilizoamuliwa kuingizwa katika Soko huru la Biashara la Afrika pamoja na kikao cha maandalizi ya mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC kupitia 'video conference' (Mwalim Nyerere Conference Centre Dar es Salaam).

**123. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeshiriki katika Mkutano wa Jukwaa la majadiliano ya Biashara ya Huduma ambalo lilijadili Rasimu ya Itifaki ya Biashara ya Huduma ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SADC). Jumuiya ya SADC bado ipo katika utekelezaji wa 'Free Trade Areas', ila wananchi katika nchi wanachama wako mbele zaidi katika hatua ya Biashara ya Huduma ambayo ni hatua ya utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Hatua hiyo imekuja ili kuwawezesha wananchi wa SADC kuwa na utaratibu wa kisheria unaotoa muongozo katika shughuli zao wanazozifanya ambapo Jumuiya ya SADC bado haijafikia hatua hiyo ya mtangamano.

**124. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeshiriki Mkutano wa Kikanda unaohusu majadiliano ya kuondosheana vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru uliofanyika Dodoma, Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC kupitia 'Video conference' uliofanyika Dar es Salaam

ambao pamoja na mambo mengine ulikabidhi Uenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa nchi ya Msumbiji na Mkutano wa SADC ulipitia muongozo wa kufuatwa kufikia uchaguzi wa kidemokrasia kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya SADC uliofanyika Dar es Salaam.

**125. Mheshimiwa Spika,** Afisi imeshiriki Mkutano wa Kikanda wa Kuondoa vikwazo visivyokuwa vya kiushuru uliofanyika Jijini Arusha. Mkutano huo ulijadili maeneo maalum yanayokwamisha utekelezaji wa Sheria ya kuondoa Vikwazo vya Biashara visivyokuwa vya kiushuru ya 2017. Maeneo hayo ikiwemo Rushwa na Uboru wa Viwango wa Bidhaa. Katika mkutano huo, Tanzania ilikuwa na msimamo wa kuondoa Rushwa isiwe sehemu ya Sheria hiyo, msimamo uliungwa mkono na Burundi, Kenya na Uganda. Aidha, Rwanda ilihitaji rushwa ijumuishwe katika Sheria hiyo. Hata hivyo, suala hilo halikupata muafaka na kuamuliwa kupelekwa mbele ya Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji kwa mazingatio yao.

**126. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeshiriki Mikutano ya kuanzisha eneo huru la biashara la Afrika (AfCFTA) uliyofanyika mjini Morogoro ambao ulijadili na kuweka msimamo wa Tanzania juu ya kufungua bidhaa zitakazoingia katika soko huru la Afrika. Soko hilo linahitaji bidhaa za asilimia 7 zifunguliwe ndani ya miaka 13, asilimia 90 zifunguliwe mara baada ya kuanza utekelezaji wa itifaki na asilimia 3 zisifunguliwe kabisa. Miongoni mwa bidhaa za Tanzania zilizofunguliwa kwenye kundi la asilimia 3 ni Karafuu kwa ajili ya kulinda zao hilo muhimu kwa uchumi wa Zanzibar na Wananchi wake.

**127. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Uratibu wa Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi itashiriki katika Mikutano ya Kikanda ndani na nje ya nchi; itajenga uelewa juu ya fursa zinazopatikana kutokana na Jumuiya za mtangamano wa Kikanda (EAC, SADC, IORA, TRIPATITE na AU); itasimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku za Afisi; itajenga uelewa kwa jamii juu ya Sera ya Diaspora Zanzibar na utekelezaji wake; itaratibu shughuli za Itifaki; itawawezesha Diaspora kushiriki katika kuchangia maendeleo ya nchi yao ya asili; itawajengea uwezo

wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi; itaanzisha na kuendeleza kanzidata (Database) ya Wanadiaspora wa Zanzibar wanaoishi Nje na ndani ya Nchi; itafanya utafiti na kutafuta mahitaji halisi ya kitaalamu yaliyopo Zanzibar hasa katika sekta ya elimu, afya na viwanda; itafanya mikutano ya mashauriano na Idara inayoshughulikia uratibu wa Diaspora kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na itashiriki katika mikutano ya ndani na kimataifa inayohusiana na Diaspora.

**128. Mheshimiwa Spika;** ili program ndogo ya Uratibu wa Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **Shilingi Mililoni Mia Nane Ishirini na Nne, Laki Tisa Hamsini na Moja Elfu** (Tshs.824,951,000) kwa ajili ya kazi za kawaida.

### **3.2.5 PROGRAMU KUU PA0705: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI.**

**Matokeo ya muda Mrefu:** Kuwa na Sheria, Sera, Programu, tafiti na Mipango endelevu itakayoimarisha uratibu, uandaaji na utekelezaji wa Sheria za Kazi, Upatikanaji wa Ajira za Staha, Uwekezaji, Ushirikiano wa Kimataifa, Uratibu wa shughuli za Wazanzibari waliopo nje ya nchi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi.

#### **3.2.5.1 Programu ndogo SA070501: Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti**

**Lengo Kuu:** Kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Sera, Sheria Mipango, Programu, Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na Tafiti za Afisi.

**129. Mheshimiwa Spika;** Programu imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya Sera ya Mafunzo Kazi ambayo inatoa muongozo wa namna ya kuendesha shughuli za Mafunzo Kazi nchini. Rasimu hiyo tayari kwa kupitiwa na vyombo vya kutoa maamuzi ikiwemo kikao cha Makatibu

Wakuu na Baraza la Mapinduzi. Pia, imefanya mapitio ya Sera ya Uwekezaji nchini ili iende sambamba na marekebisho ya Sheria Nambari 14 ya mwaka 2018 ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar iliyoongezwa jadweli nambari 3 na 6 la kuimarisha vivutio vya uwekezaji maalum wa kimkakati kwa kisiwa cha Pemba. Aidha, nakala 100 za Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2019 na nakala 40 za toleo pendwa la Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2019 zimechapishwa na kugaiwa kwa Wadau.

**130. Mheshimiwa Spika;** Imeratibu mapitio ya Sheria za Afisi kujiridhisha kama bado zinaendana na wakati ama zimepitwa na wakati. Sheria zilizobainika kuwa na mapungufu na zinahitaji marekebisho ni pamoja na Sheria ya Ajira namba 11 ya mwaka 2005, Sheria ya Mahusiano Kazini namba 1 ya mwaka 2005; Sheria ya Usalama na Afya Kazini namba 8 ya mwaka 2005 na Sheria ya Fidua kwa Wafanyakazi namba 15 ya 1986 ambazo bado zinaendelea na marekebisho katika Tume ya Kurekebisha Sheria. Sheria ya Fidua imeonekana inahitaji kuandikwa upya ili iweze kutoa Muongozo wa uendeshaji wa Mfuko wa Fidua ambao uko katika hatua ya kuanzishwa. Vile vile, imefanyiwa mapitio ya Sheria ya Mashirikiano ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi namba 8 ya mwaka 2015 ambayo marekebisho yake yamekamiliwa na Sheria ya Masuala ya Diaspora namba 4 ya mwaka 2020 ipo katika hatua ya kujadiliwa na Wadau.

**131. Mheshimiwa Spika;** Programu imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo watendaji 30 wa Afisi juu ya masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini. Mafunzo hayo yalikuwa ni ya kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Afisi, kuandaa nyenzo ya kufanya ufuatiliaji na uandaaji wa taarifa za utekelezaji wa shughuli za Afisi unafanywa kwa mujibu wa nyenzo zilizoandaliwa. Pia, imefanya ziara za ufuatiliaji Unguja na Pemba katika miradi ya ZIPA, Kituo cha Incubation, Vikundi vilivyopewa mikopo, vikundi vya Ushirika, Kituo cha Barefoot na nyumba zilizoufaika na kuwekewa taa za umeme wa jua ili kubaini mafanikio na changamoto za kiutendaji. Taarifa za ziara hizo zinawasilishwa Idara husika ili kuzifanyia kazi changamoto zilizogundulikana. Miongoni mwa changamoto ni

pamoja na miundombinu hafifu katika maeneo ya uwekezaji, ukosefu wa mitaji, masoko na mafunzo kwa wajasiriamali.

**132. Mheshimiwa Spika;** Programu inaendelea na uimarishaji wa Kitengo cha TEHAMA ili kiendane na kasi ya Awamu ya Nane. Miongoni mwa maboresho yaliyofikiwa ni pamoja na kuanzisha mitandao ya kijamii ambayo inawawezesha wananchi kutoa maoni yao moja kwa moja kwa mujibu wa shughuli zinazofanyika pamoja na kupata matukio mbali mbali ya Afisi. Hivi sasa, Afisi imeanza kurusha shughuli tofauti zinazotekelezwa na Afisi ili wananchi wayatambue majukumu ya Afisi na kuweza kufuatilia upatikanaji wa huduma zinazotolewa na Afisi. Aidha, tumeanzisha Tovuti ya Ofisi ambayo inatoa taarifa na Makala zinazotayarishwa na Afisi. Vile vile, imeandaa habari 200 na vipindi 27 vya televisheni na redio ambavyo vimerushwa hewani kupitia ZBC redio na TV, Zanzibar Cable, Chuchu FM, Bahari FM, Zenj FM, Hits FM, Zanzibar leo, Island TV, Zanzibar Cable, On line TV, TBC redio na TV pamoja na ITV. Pia, imeandaa makala 7 na kuzitoa katika Gazeti la Daily News, Nipashe, The Guardian, Majira, Mwenge, Uhuru, Mwananchi na Habari leo.

**133. Mheshimiwa Spika;** Kutokana na mabadiliko ya muundo wa Serikali, Afisi inaendelea na uandaaji wa Mpango Mkakati ili uende sambamba na mageuzi ya Afisi yaliyofanyika hivi karibuni. Utayarishaji wa Mkakati huo unazingatia Muongozo wa utayarishaji uliotolewa na Tume ya Mipango pamoja na kuzingatia Sera za Kitaifa ikiwemo Dira 2050, Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020 – 2050 na Maagizo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia, imeratibu zoezi la kuandaa Mpango Kazi wa miaka mitano wa utekelezaji wa Programu za Afisi kwa kuzingatia nyenzo zilizotajwa hapo juu pamoja na uandaaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Afisi kwa miaka 5 ambapo jumla ya miradi 25 ilibuniwa na kuwasilishwa Tume ya Mipango na Wafadhili kwa kupatiwa fedha za utekelezaji.

**134. Mheshimiwa Spika;** Afisi imeanza kuratibu utengenezaji wa Muongozo wa Uwekezaji Zanzibar kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Programu za Maendeleo (UNDP) kwa lengo la kukuza

Sekta ya Uwekezaji nchini na kuimarisha mazingira mazuri kwa wawekezaji wa ndani na nje ili kuzielewa fursa zilizopo za uwekezaji katika sekta mbali mbali ikiwemo Sekta ya Uchumi wa Buluu, Mafuta na Gesi pamoja na maeneo mengine ya uwekezaji yaliyopo. Kamati maalum imeundwa inayoshirikiana na Mtaalamu Muelekezi kuandaa Muongozo huo. Kamati imeanza kuandaa fursa na maeneo ya uwekezaji yaliyopo katika sekta zao.

**135. Mheshimiwa Spika;** Programu Kwa kushirikiana na Idara ya Afya na Usalama Kazini inaendelea kuratibu ufanyaji wa Utafiti wa kuyatambua maradhi yatokanayo na Kazi na rasimu ya matokeo ya mwanzo ya utafiti huo yameshawasilishwa ambapo matokeo yanaonyesha kwamba asilimia 39 ya waliohojiwa wana magonjwa yatokanayo na kazi na asilimia 22 wameumia kazini. Pia, ulibaini kwamba asilimia 57 ya wanaopata magonjwa yatokanayo na kazi na asilimia 35 wanaoumia kazini wanajilipia matibabu wao wenyewe. Aidha, Utafiti unaonyesha kuwa asilimia 78 ya wanaopata magonjwa yatokanayo na kazi na asilimia 75 wanaoumia kazini wanaendelea na majukumu yao sehemu zile zile za kazi. Pia, matokeo yamebaini kwamba madaktari wachache na madaktari wasaidizi (asilimia 14) ndio wenye uelewa juu ya maradhi yatokanayo na kazi pamoja na taratibu za kufuata ili mhanga kupata fidia. Sekta zilizofanyiwa utafiti huu ni pamoja na sekta ya afya, elimu, utalii na ujenzi (majengo na barabara).

**136. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Program ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti itafanya mapitio ya Sera 4 na kukamilisha uandaaji wa Sera ya Mafunzo Kazi, itakamilisha mapitio ya Sheria ya Ajira namba 11 ya mwaka 2005; Sheria ya Mahusiano Kazini namba 1 ya mwaka 2005; Sheria ya Usalama na Afya Kazini namba 8 ya mwaka 2005 na Sheria ya Masuala ya Diaspora namba 4 ya mwaka 2020; itafanya tafiti za Afisi kwa mujibu wa ajenda za Utafiti za Afisi; itaratibu utekelezaji wa program na miradi ya Afisi; itafanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi; itaimarisha mfumo wa TEHAMA na upatikanaji wa habari na taarifa za Afisi; itaimarisha upatikanaji wa takwimu za shughuli mbali mbali za Afisi na itaimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa na Afisi.

**137. Mheshimiwa Spika;** ili Program ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **Shilingi Biloni Sita, Milioni Mia Moja na Tatu, Laki Tatu Thalathini na Tano Eflu** (Tshs.6,103,335,000) kwa ajili ya kazi za kawaida na maendeleo.

### **3.2.5.2 Programu ndogo SA070502: Utawala na Uendeshaji**

**Lengo Kuu:** Kukuza uwezo wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**138. Mheshimiwa Spika;** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi na ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Uendeshaji na Utumishi za Afisi.

**139. Mheshimiwa Spika;** Programu imesimamia ulipaji wa maposho ya likizo kwa wafanyakazi 35 na malipo ya muda wa ziada kwa wafanyakazi 27. Vile vile, imefuatilia malipo ya kiinua mgongo kwa Wastaafu 10 (Wanaume 5 na Wanawake 5) Unguja.

**140. Mheshimiwa Spika;** Kupitia fomu za Upimaji Utendaji kazi wa Watumishi (Performance appraisal) imewafanyia tathmini Wafanyakazi 96 (Wanawake 56 na Wanaume 40) juu ya uwezo wa utendaji kazi wao ili kuweza kupatiwa nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma No. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2014.

**141. Mheshimiwa Spika;** Afisi imefanya marekebisho ya Mkataba wa Utoaji wa huduma kwa Mteja baada ya mabadiliko ya Muundo wa Afisi katika Awamu ya nane. Pia, imefanya malipo ya bima kwa gari 6 za Afisi kama agizo la Serikali linavyoelekeza pamoja na kuzifanyia matengenezo na ukaguzi wa kawaida wa kiufundi gari 5. Aidha, imeendelea kulipia gharama za umeme, maji na vifaa vya usafi.

**142. Mheshimiwa Spika;** Afisi imelipia ada ya Mafunzo ya Awali "Induction Course" kwa Wafanyakazi Arobaini na Mbili (42) (Wanaume 9

na Wanawake 33). Pia, imelipia ada Wafanyakazi (54) ambao watahudhuria mafunzo hayo kwa awamu. Aidha, inaendelea kuwasaidia ada za masomo wafanyakazi watano (5); Mfanyakazi mmoja (1) ngazi ya Shahada ya Pili, Wafanyakazi watatu (3) ngazi ya Shahada ya Kwanza na mmoja (1) ngazi ya Stashahada. Pia, imeendelea kugharamia safari za ndani kwa Viongozi na Maafisa wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ili kuweza kushiriki Mikutano, Warsha, Semina na Mokongamano mbali mbali ya Kitaifa.

**143. Mheshimiwa Spika;** Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia Program ya Utawala na Uendeshaji itasimamia Maslahi ya Wafanyakazi kama vile malipo ya mishahara, posho la likizo, malipo ya saa za ziada, malipo ya ubani kwa wafiwa pamoja na kuandaa na kufuatilia malipo ya viinua mgongo kwa Wastaafu wetu; itaendelea kutoa mafunzo ya ndani na mafunzo ya awali kwa wafanyakazi wapya walioajiriwa; itaendelea na zoezi la Upimaji Utendaji kazi kwa Wafanyakazi wake kila ambapo wanapostahiki kufanyiwa; itasimamia ununuzi wa Genereta la Dharura pale Umeme Unapokatika pamoja na kununua vifaa na vitendea kazi; itaandaa Mpango wa Mafunzo na Mpango wa Rasilimali watu na itaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa Wafanyakazi wa idara zote zilizomo ndani ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa lengo la kwenda sambamba na Mpango mkakati wa Rasilimali watu 2017/2022 wa Afisi na Taasisi zilizomo ndani yake.

**144. Mheshimiwa Spika;** ili program ndogo ya Utawala na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tisa Sabini na Sita, Laki Tano Thalathini na Sita Eflu** (Tshs.1,976,536,000) kwa kazi za kawaida.

### **3.2.5.3 Programu ndogo SA070503: Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Wizara Pemba.**

**Lengo Kuu:** Kuratibu na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Afisi kwa upande wa Pemba.

**145. Mheshimiwa Spika;** Programu ndogo hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba ambayo inahusisha shughuli za Idara ya Uendeshaji na Utumishi pamoja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

**146. Mheshimiwa Spika;** Programu imewasaidia ada za masomo wafanyakazi wawili (2) kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Shahada ya Pili katika fani ya Teknolojia ya Habari na fani ya Uongozi wa Umma. Pia, imewawezesha wafanyakazi watano (5) (wanaume 4 na mwanamke 1) waliostaafu kushiriki mafunzo kwa ajili ya kujiandaa kustaafu, kuwafanyia sherehe na kuwapa zawadi kwa ajili ya kuwaaga. Mafunzo ya kustaafu yanasimamiwa na (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Chuo cha Utawala wa Umma Zanzibar (IPA).

**147. Mheshimiwa Spika;** Afisi imelipa fedha za likizo kwa wafanyakazi 16 (Wanawake 9 na Wanaume 7) na wafanyakazi 12 wamelipwa posho la masaa ya ziada. Imefanya manunuzi ya magazeti ya kila siku pamoja na kulipia gharama za safari kikazi, umeme, maji, mafuta na huduma za mtandao. Pia, imefanya matengenezo ya vyombo vya moto vitatu (3) pamoja na kulipia bima gari mbili (2) na vespa moja (1). Kadhalika, imefanya malipo ya huduma za usafi kwa kampuni inayotoa huduma za usafi wa ndani ya Afisi.

**148. Mheshimiwa Spika;** Afisi imefanya ziara tatu (3) za ufuatiliaji na tathmini kwa madhumuni ya kuboresha utendaji wa shughuli za Afisi. Afisi imefanya ufuatiliaji kutambua watu wanaoishi mazingira magumu. Pia, imefanya ufuatiliaji wa vikundi vilivyowezeshwa na Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Idara ya Maendeleo ya Ushirika na kuona kwa ujumla vikundi hivyo vinaendelea na shughuli zao vizuri

kwani mikopo na taaluma walioipata imewasaidia kutatua baadhi ya changamoto zinazowakabili.

**149. Mheshimiwa Spika;** Afisi imefanya ufuatiliaji katika Skuli binafsi na Kampuni ya Sino Hydro inayojishughulisha na ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji kwa lengo la kutambua ufanisi na changamoto katika taasisi hizo kwenye masuala ya usalama na afya kazini pamoja na haki na maslahi kwa wafanyakazi. Miongoni mwa changamoto zilizobainika ni kutokuwa na mikataba ya kazi kwa wafanyakazi na kutochunguzwa kwa afya za wafanyakazi wakati wa kuajiriwa. Changamoto hizi Afisi kupitia Kamisheni ya Kazi, Idara ya Ajira na Idara ya Usalama na Afya kazini tayari imeshazifanyia kazi kwa kutoa Agizo kwa taasisi hizo ili kutatuliwa kwa changamoto zilizojitokeza. Pia, imeratibu uandaaji wa ripoti mbalimbali za utekelezaji ikiwemo ripoti ya utekelezaji wa bango kitita, Ripoti za utekelezaji za ilani ya uchaguzi, Utayarishaji wa mpangokazi wa miaka mitano wa 2020/21 – 2024/25, pamoja na utayarishaji wa mpango wa bajeti wa muda wa kati wa Wizara (MTEF) kwa kipindi cha 2021/22 – 2023/24.

**150. Mheshimiwa Spika;** kwa mwaka wa Fedha 2021/2022, Program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba itaendelea kusimamia maslahi ya wafanyakazi; itasimamia utoaji wa mafunzo ya ndani na mafunzo ya awali; itaratibu utekelezaji wa Sera na Sheria mbali mbali za Afisi; itaandaa taarifa za utekelezaji na kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za Afisi; itaratibu utekelezaji wa Programu na miradi pamoja kuripoti utekelezaji wake kunakohusika.

**151. Mheshimiwa Spika;** ili program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Afisi Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022, naliomba Baraza lako kuidhinisha jumla ya **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Mbili Sabini na Mbili, Laki Tano Ishirini na Tano Eflu** (Tshs.1,272,525,000) kwa kazi za kawaida.

#### **4.0 MAOMBI YA FEDHA KWA PROGRAMU ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**152. Mheshimiwa Spika,** Ili Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 naliomba Baraza lako liidhinishhe jumla ya **Shilingi Bilioni Thalathini na Nne, Milioni Mia Nane Ishirini na Tisa na Laki Sita** (Tshs.34,829,600,000). Kati ya hizo **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Moja Sabini na Sita na Laki Sita** (Tshs.5,176,600,000) ni Mishahara; **Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mbili** (Tshs.6,002,000,000) ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida; **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Sita Thamanini na Sita, Laki Sita** (Tshs.2,686,600,000) kwa ajili ya ruzuku na **Shilingi Bilioni Ishirini, Milioni Mia Tisa Sitini na Tano** (Tshs.20,965,000,000) kwa ajili ya matumizi ya miradi ya Maendeleo.

**153. Mheshimiwa Spika;** Mgawanyo wa fedha hizo kiprogramu ni kama ufuatao:- **Shilingi Bilioni Tano, Milioni Tano, Laki Nane Thamanini na Saba Eflu** (Tshs.5,005,887,000) ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu Shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu; **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili Thalathini na Sita na Laki Tisa** (Tshs. 2,236,900,000) kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote; **Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Sita Thalathini na Nne, Laki Nane Kumi na Sita Eflu** (Tshs.7,634,816,000) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; **Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tano Tisini na Tisa, Laki Sita na Eflu Moja** (Tshs.10,599,601,000) kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Kuimarisha Uwekezaji na Shughuli za Serikali Kikanda na Kimataifa na **Shilingi Bilioni Tisa, Milioni Mia Tatu Hamsini na Mbili, Laki Tatu Tisini na Sita Eflu** (Tshs.9,352,396,000) zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji (**Kiambatanisho nambari 7 kinahusika**).

**154. Mheshimiwa Spika;** Afisi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 inatarajiwa kukusanya mapato ya **Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nane Thalathini na Tano na Laki Sita** (Tshs.2,835,600,000) kutokana na Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi (**Kiambatanisho nambari 8 kinahusika**).

## **5.0 HITIMISHO**

**155. Mheshimiwa Spika;** Afisi inatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na Watendaji mbali mbali ikiwemo taasisi za Serikali, taasisi za kiraia na Washirika wa Maendeleo. Miongoni mwa Washirika wa Maendeleo tunaofanya kazi nao ni pamoja na ILO, UNIDO, MIVARF, UNDP, COSTECH, Milele Foundation, FAO, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) na Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**156. Mheshimiwa Spika;** Pia, Afisi inafanya kazi na Taasisi za Kiraia na inazishukuru Taasisi zote inazoshirikiana nazo. Pia, inazishukuru taasisi zote za kifedha, ikiwemo PBZ kwa mashirikiano yao mazuri na Afisi.

**157. Mheshimiwa Spika;** Napenda kuvishukuru vyombo vya habari vya Serikali na Binafsi kwa jitihada kubwa wanayoichukua ya kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazofanywa na Afisi ikiwemo kuwahamasisha vijana kuwa na moyo wa kujiajiri wenyewe badala ya kutegemea ajira kutoka Serikalini na kukuza uwekezaji nchini. Vyombo hivyo ni pamoja na ZBC redio na televisheni, Gazeti la Zanzibar Leo, Zanzibar Cable televisheni, TBC, AZAM TV, Zenj FM, Island TV na Hits FM. Ni vigumu kuvitaja vyote lakini napenda kuvishukuru vyombo vyote vya habari vilivyoshirikiana nasi.

**158. Mheshimiwa Spika;** Pia, napenda kumshukuru kwa mara nyengine tena Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwa nasi kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yetu. Tunamuomba azidi kutupa muongozo na maelekezo

yatakayoongeza ufanisi wa shughuli zetu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza Wawekezaji wote waliowekeza na walioonyesha nia ya kuwekeza Zanzibar. Nawaahidi hawatojuta kwa uamuzi walioufanya kwani Serikali inaendelea kuweka mazingira mazuri ya Uwekezaji. Vile vile, Nakupongeza tena Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Uchumi ya Baraza, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti pamoja na Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali kwa michango na maelekezo yaliyopelekea kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

**159. Mheshimiwa Spika;** Mwisho kabisa napenda kuwapongeza watendaji wote wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mashirikiano makubwa ya kiutendaji wanayonipa katika kutekeleza majukumu ya Afisi. Mafanikio tunayoyapata ni kutokana na utendaji wao mahiri na mashirikiano mazuri baina yetu. Namshukuru sana Katibu Mkuu Ndugu Mussa Haji Ali, Kamishna wa Kazi, Afisa Mdhamini Pemba, Wakurugenzi na Watendaji wa ngazi zote. Namuomba Mwenyezi Mungu adumishe mapenzi na mashirikiano baina yetu katika kuwatumikia wananchi na kutekeleza majukumu yetu.

**160. Mheshimiwa Spika;** Naliomba Baraza lako lipokee, lijadili, litushauri na hatimae liipitishie Bajeti hii.

**161. Mheshimiwa Spika;** Naomba kutoa hoja.

Ahsanteni

.....  
**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA(MBM)**  
**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI**  
**ZANZIBAR**

## VIAMBATANISHO

### Kiambatanisho Nambari 1.

#### PROGRAMU KUU NA NDOGO ARKUU

<b>PA0701: Programu Kuu ya Kusimamia Huduma na Kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu</b>
SA070101: Program Ndogo ya Kusimamia huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais.
SA070102: Programu Ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi.
<b>PA0702: Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote.</b>
SA070201: Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha.
SA070202: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini.
SA070203: Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kimatatifa na Majadiliano ya Pamoja Kazini
<b>PA0703: Programu Kuu ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi.</b>
SA070301: Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi.
SQ070302: Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika
SQ070303: Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezesaji Wananchi Kiuchumi.
<b>PA0704: Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Shughuli za Serikali Kikanda na Kimataifa</b>
SA070401: Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji
SA070402: Programu Ndogo ya Mashikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi
SA070403: Programu Ndogo ya Uratibu wa Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi
<b>PA0705: Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.</b>
SA070501: Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti
SA070502: Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji
SA070503: Programu Ndogo ya Uratibu na Utekezaji wa Shughuli za Wizara Pemba

**Kiambatanisho Nambari 2.**

**MUHTASARI WA UPATIKANAJI WA FEDHA JULAI 2020 HADI MACHI, 2021**

Programu	Makadirio ya Mwaka 2020/2021	Kilichopangwa Julai- Machi 2021	Kilichopatikana Julai – Machi 2020	Asilimia ya fedha kwa Julai-Machi 2021	Asilimia ya fedha kwa Mwaka 2020/2021
<b>Programu Kuu ya Kusimamia Huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na kuimarisha Mawasiliano Ikulu</b>	4,222,795,000	3,336,868,546	2,462,407,158	74	58
Programu Ndogo ya Kusimamia huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais	3,756,928,000	2,855,407,627	2,240,994,297	78	60
Programu Ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi	465,867,000	481,460,918	221,412,861	46	48
<b>Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote</b>	<b>1,478,900,000</b>	<b>1,181,996,092</b>	<b>630,339,280</b>	55	43
Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha	224,452,380	210,943,568	42,687,009	41	36
Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini	206,307,320	150,637,063	33,772,635	39	28
Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja	1,048,140,300	820,415,461	553,879,636	58	45
<b>Programu Kuu ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi</b>	<b>2,285,136,548</b>	<b>2,121,121,003</b>	<b>642,033,269</b>	30	28
Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi	280,446,724	258,630,234	144,867,452	56	52
Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika	379,967,112	293,237,057	256,464,203	87	67
Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezesaji Wananchi Kiuchumi	1,624,722,712	1,569,253,713	240,701,614	15	15
<b>Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Shughuli za Serikali Kikanda na Kimataifa</b>	<b>1,710,315,450</b>	<b>1,163,554,411</b>	<b>699,521,931</b>	60	41
Programu Ndogo ya Maendeleo ya Ukuaji wa Uchumi kupitia Uwekezaji	866,992,680	511,675,993	434,796,900	85	50
Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi	100,000,000	101,632,909	56,073,776	55	56
Programu Ndogo Uratibu wa Ushirikiano wa Kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi	743,322,770	550,245,509	208,651,255	38	28
<b>Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.</b>	<b>4,692,620,356</b>	<b>2,487,186,535</b>	<b>2,985,306,110</b>	77	64
Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Tafiti	1,888,061,216	370,198,017	1,634,544,899	92	87
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji	1,938,035,480	1,437,070,861	858,540,355	60	44
Programu Ndogo ya Uratibu na Utekezaji wa Shughuli za Wizara	866,523,660	679,917,657	492,220,856	72	57
<b>Jumla Kuu</b>	<b>14,389,767,354</b>	<b>8,207,262,677</b>	<b>7,419,607,748</b>	64	52

**Kiambatanisho Nambari 3.**

**MUHTASARI WA MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2020 HADI MACHI, 2021**

<b>PEMBA</b>				
<b>KASMA</b>	<b>MAELEZO</b>	<b>KILICHOPANGWA</b>	<b>KILICHOKUSANYWA</b>	<b>ASILIMIA</b>
1422012	Malipo ya Ukaguzi katika Sehemu ya Kazi	20,000,000	1,230,000	6
1422036	Ada ya Uandikishaji wa Vyama vya Ushirika	9,000,000	3,530,000	39
1422037	Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma	9,000,000	4,215,000	47
1422071	Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi	15,000,000	2,255,000	15
	<b>JUMLA PEMBA</b>	<b>53,000,000</b>	<b>11,230,000</b>	<b>21</b>
<b>UNGUJA</b>				
<b>KASMA</b>	<b>MAELEZO</b>	<b>BAJETI</b>	<b>HALISI</b>	<b>ASILIMIA</b>
1422036	Ada ya Uandikishaji wa Vyama vya Ushirika	21,000,000	3,260,000	16
1422037	Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma	21,000,000	9,457,947	45
1422075	Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira za Nje	108,555,000	41,450,000	38
1422011	Vibali vya Kazi kwa Wataalamu wa Kigeni	950,000,000	429,674,630	45
1422012	Malipo ya Ukaguzi katika Sehemu ya Kazi	841,847,000	32,825,150	4
1422071	Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi	83,153,000	39,820,000	48
	<b>JUMLA UNGUJA</b>	<b>2,025,555,000</b>	<b>556,487,727</b>	<b>27</b>
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>2,078,555,000</b>	<b>667,787,727</b>	<b>32</b>

**Kiambatanisho Nambari 4.**

**UTOAJI WA MIKOPO YA MFUKO WA UWEZESHAJI KUANZIA JULAI 2020 HADI MACHI, 2021**

Na.	WILAYA	IDADI YA MIKOPO	VIKUNDI	BINAFSI	SHEHIA	FEDHA ZILIZOTOLEWA	WALIONUFAIKA		JUMLA
							W'KE	W'ME	
1	CHAKE CHAKE	62	30	32	22	61,400,000	498	301	799
2	MKOANI	64	13	51	12	45,500,000	129	123	252
3	WETE	66	34	32	14	58,500,000	450	79	529
4	MICHEWENI	52	11	41	11	47,500,000	112	129	241
	<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>244</b>	<b>88</b>	<b>156</b>	<b>59</b>	<b>221,900,000</b>	<b>1189</b>	<b>632</b>	<b>1821</b>
5	MJINI	60	12	48	23	65,700,000	142	132	274
6	MAGHARIBI A	50	07	43	15	55,675,000	96	116	212
7	MAGHARIBI B	63	14	49	17	101,750,000	285	291	576
8	KASKAZINI "A"	49	08	41	19	45,100,000	119	110	229
9	KASKAZINI "B"	53	08	45	11	45,600,000	93	87	180
10	KATI	49	06	43	21	52,700,000	119	107	226
11	KUSINI	49	13	36	12	49,000,000	190	132	322
	<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>373</b>	<b>68</b>	<b>305</b>	<b>118</b>	<b>415,525,000</b>	<b>1044</b>	<b>975</b>	<b>2019</b>
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>617</b>	<b>156</b>	<b>461</b>	<b>177</b>	<b>637,425,000</b>	<b>2233</b>	<b>1607</b>	<b>3840</b>

**Kiambatanisho nambari 5**

**MCHANGANUO WA UTOAJI WA MIKOPO KWA MAKUNDI MAALUM 2020/2021**

<b>A</b>	<b>VIJANA</b>				
	Jina la kikundi	Shehia	Wilaya	Shughuli	Fedha
1	Sarifa njema Business	Nunwi	Kaskazini A	MINI SUPERMARKET	5,000,000
2	Hill View spice	KJizimbani	Wete	Usarifu wa bidhaa za viungo	2,000,000
3	Atowae ni Karima	Kengeja	Mkoani	Kazi za mikono/ welding	1,500,000
4	MECO COOPERATIVE	Mtemani	Wete	Mkahawa	1,500,000
5	Tumshukuru Mungu	Mwambe	Mkoani	Kilimo matundu na mbogamboga	3,000,000
6	Vijana na Maendeleo	canjaani	Chake Chake	Ufumaji na Ushonaji	2,000,000
7	Sum Printing Partnership	Mwanakwerekwe	Mjini	Duka la vifaa vya ofisi/skuli	5,000,000
8	Nguvu hazichezewi	Mivumoni	Chake Chake	Uzalishaji chumvi	1,500,000
9	Kheri Tunaomba	Kibeni	Kaskazini A	Kilimo na Ufugaji	5,000,000
10	Professional Sc & technology	Amani	Mjini	Duka la Vyakula Jumla na Rejajreja	4,000,000
		<b>Jumla</b>			<b>30,500,000</b>
<b>B</b>	<b>WATU WENYE ULEMAVU/MAKUNDI MAALUM</b>				
1	SABU SPICE	Kijichi	Magharibi A	Usarifu wa matunda na viungo	8,500,000
2	UWUKO	Konde	Micheweni	Utengenezaji Sabuni	5,000,000
3	Time Ramadan	Majenzi	Micheweni	Utengenezaji wa bidhaa za Usumba	500,000
4	Kassim Khamis Ali	Majenzi	Micheweni	Uwakala wa mitandao ya simu	1,500,000
		Jumla			15,500,000
<b>C</b>	<b>WANAWAKE</b>				
1	Tunaweza B. Group	Amani	Mjini	Biashara ya Vitoweo	3,000,000

2	Tupe Salama	Mwanakwerekwe	Magharibi B	Usarifu wa matunda	5,000,000
3	Wapendanao	Kwa Mchina	Magharibi B	Biashara ya kukopeshana	5,000,000
4	HAKUNA Majungu	Jitimai	Magharibi B	Ufumaji	2,000,000
5	Tushikamame Co op	Wingwi Kipange	Micheweni	Ufinyanzi	4,000,000
6	Subira ina Malipo Coop	Mkataleni	Kaskazini B	Kilimo na ufugaji	4,000,000
7	Elimu ni Ufunguo	Tibirinzi	Chake Chake	Ufumaji na Ushonaji	1,500,000
8	Jambo Nia Co operative	Wawi	Chake Chake	Utengenezaji sabuni za vipande	3,000,000
9	Ushirika wa ZIWARDE	Rahaleo	Mjini	Utengenezaji sabuni za vipande ,Saluni	3,000,000
10	SHARILY PARTNERSHIP	Mchangani	Mjini	Duka la Nguo	3,000,000
11	Subira Ina Mpaka	Mkele	Mjini	Duka la Vyakula	2,000,000
12	Kikundi jamatul kheir	Mlandege	Mjini	Biashara ya Magodoro	5,000,000
13	Jambo Jema	Mtende	Kusini	Ufugaji Kuku wa Nyama na Mayai	4,500,000
14	WANAWAKE NA MAENDELEO	BUBUBU	Magharibi A	Biashara Mchanganyiko	8,500,000
15	HATUNA SIMANZI GROUP	BUBUBU	Magharibi A		4,000,000
16	Tupe Nia C cooperative	Mkokotoni	Kaskazini A	Biashara Mchangaanyiko	3,100,000
17	Mpatifu hajisifu	Sizini	Micheweni	Usarifu wa Kamba	2,000,000
18	Mwanzo Mgumu C oop	Mkoroshoni	Chake Chake	Duka la nguo	2,000,000
19	Subira ina Malipo Coop	Mkataleni	Kaskazini B	Kilimo na ufugaji	3,800,000
20	Tupo Tayari Co operative	Shauri Moyo	Mjini	Ukaushaji madagaa	3,000,000
21	Ukipewa shukuru Mungu	Makangale	Micheweni	Uvunaji mazao ya Baharini/Uvuvi	4,000,000
		<b>Jumla</b>			<b>76,600,000</b>

**Kiambatanisho Nambari 6.**

**MAREJESHO YA MIKOPO MFUKO WA UWEZESHAJI KUANZIA JULAI 2020 HADI MACHI, 2021**

<b>Wilaya</b>	<b>Julai 2020</b>	<b>Agosti 2020</b>	<b>Septemba 2020</b>	<b>Oktoba 2020</b>	<b>Novemba 2020</b>	<b>Disemba, 2020</b>	<b>Januari 2021</b>	<b>Februari 2021</b>	<b>Machi, 2021</b>	<b>JUMLA</b>
CHAKE	5,643,000	5,258,000	6,886,000	3,552,000	2,416,000	2,789,000	2,712,000	4,009,000	3,086,000	36,351,000
MKOANI	837,000	2,999,000	2,058,000	1,383,800	2,666,000	1,883,600	2,240,000	2,526,000	2,266,000	18,859,400
WETE	4,137,000	3,045,000	3,244,000	1,727,000	1,490,000	2,446,000	3,404,000	1,929,000	3,361,000	24,783,000
M/WENI	2,267,800	3,157,000	3,363,000	1,293,400	3,284,000	2,890,000	2,277,600	860,000	3,249,000	22,641,800
J. NDOGO	12,884,800	14,459,000	15,551,000	7,956,200	9,856,000	10,008,600	10,633,600	9,324,000	11,962,000	102,635,200
MJINI	2,500,000	2,251,000	4,261,000	1,744,000	3,437,000	1,637,000	4,112,000	4,334,000	3,335,000	27,611,000
MAGH A	3,105,000	3,420,000	4,895,000	3,058,000	4,145,000	3,905,000	4,950,000	5,943,500	5,190,000	38,611,500
MAGH.B	4,744,000	4,670,000	7,473,000	4,976,000	5,629,000	4,875,000	4,981,000	5,456,000	4,901,000	47,705,000
KASK "A"	3,200,000	2,390,000	2,851,000	2,270,000	2,515,000	3,839,000	2,560,000	2,403,500	2,368,000	24,396,500
KASK "B"	1,725,000	825,000	2,505,000	1,159,000	1,615,000	855,000	2,560,000	1,720,000	2,310,000	15,274,000
KATI	3,385,000	2,207,000	4,265,000	2,177,000	3,304,000	3,167,500	2,905,000	4,625,000	3,050,000	29,085,500
KUSINI	2,800,000	3,351,000	3,140,000	2,375,000	2,207,000	2,155,000	2,445,000	4,439,000	1,720,000	24,632,000
J.NDOGO	21,459,000	19,114,000	29,390,000	17,759,000	22,852,000	20,433,500	24,513,000	28,421,000	22,874,000	207,315,500
<b>J.KUU</b>	<b>34,343,800</b>	<b>33,573,000</b>	<b>44,941,000</b>	<b>25,715,200</b>	<b>32,708,000</b>	<b>30,442,100</b>	<b>35,146,600</b>	<b>37,745,000</b>	<b>34,836,000</b>	<b>309,950,700</b>

**Kiambatisho Nambari 7.**

**MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

<b>Programu</b>	<b>MATUMIZI YA KAWAIDA (OC)</b>	<b>MISHAHARA</b>	<b>RUZUKU</b>	<b>MAENDELEO</b>	<b>JUMLA</b>
<b>Programu Kuu ya Kusimamia Huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais na kuimarisha Mawasiliano Ikulu</b>	<b>2,200,000,000</b>	<b>2,305,887,000</b>		<b>500,000,000</b>	<b>5,005,887,000</b>
Programu Ndogo ya Kusimamia huduma na kuratibu shughuli za Mheshimiwa Rais	1,800,000,000	2,153,975,000			3,953,975,000
Programu Ndogo ya Kuimarisha Mawasiliano baina ya Serikali na Wananchi	400,000,000	151,912,000		500,000,000	1,051,912,000
<b>Programu Kuu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa Wote</b>			<b>1,736,900,000</b>	<b>500,000,000</b>	<b>2,236,900,000</b>
Programu Ndogo ya Uratibu wa Upatikanaji wa Ajira za Staha			120,000,000	500,000,000	620,000,000
Programu Ndogo ya Usimamizi wa Usalama na Afya Kazini			120,000,000		120,000,000
Programu Ndogo ya Usimamizi wa Viwango vya Kazi vya Kitaifa na Majadiliano ya Pamoja			1,496,900,000		1,496,900,000
<b>Programu Kuu ya Uwezesaji Wananchi Kiuchumi</b>	<b>800,000,000</b>	<b>678,616,000</b>	<b>191,200,000</b>	<b>5,965,000,000</b>	<b>7,634,816,000</b>
Programu Ndogo ya Mfuko wa Uwezesaji Wananchi Kiuchumi		127,007,000	191,200,000		318,207,000
Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Vyama vya Ushirika	300,000,000	366,750,000			666,750,000
Programu Ndogo ya Uratibu na Uendelezaji wa Programu za Uwezesaji Wananchi Kiuchumi	500,000,000	184,859,000		5,965,000,000	6,649,859,000
<b>Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano Bina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma</b>	<b>1,000,000,000</b>	<b>341,101,000</b>	<b>758,500,000</b>	<b>8,500,000,000</b>	<b>10,599,601,000</b>
Programu Ndogo ya Kushajiisha Uwekezaji wa ndani na nje ya nchi			758,500,000	7,500,000,000	8,258,500,000
Programu Ndogo ya Mashirikiano Baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma	350,000,000	166,150,000		1,000,000,000	1,516,150,000
Programu Ndogo Kuratibu Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa kwa Wazanzibari Wanaoishi nje ya Nchi	650,000,000	174,951,000			824,951,000
<b>Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji</b>	<b>2,002,000,000</b>	<b>1,850,396,000</b>		<b>5,500,000,000</b>	<b>9,352,396,000</b>
Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango Sera na Tafiti	452,000,000	151,335,000		5,500,000,000	6,103,335,000
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji	1,000,000,000	976,536,000			1,976,536,000
Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba	550,000,000	722,525,000			1,272,525,000
<b>JUMLA KUU</b>	<b>6,002,000,000</b>	<b>5,176,000,000</b>	<b>2,686,600,000</b>	<b>20,965,000,000</b>	<b>34,829,600,000</b>

**Kiambatanisho Nambari 8.**

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

<b>PEMBA</b>				
<b>KASMA</b>	<b>MAELEZO</b>	<b>MAKADIRIO 2021-2022</b>	<b>MAKISIO 2022-2023</b>	<b>MAKISIO 2023-2024</b>
1422012	Uthibitishwaji wa Mikataba ya Kazi	50,000,000	60,000,000	70,000,000
1422036	Ada ya Uandikishaji wa Vyama vya Ushirika	15,000,000	15,000,000	15,000,000
1422037	Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma	15,000,000	15,000,000	15,000,000
1422071	Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi	35,000,000	50,000,000	65,000,000
	<b>JUMLA PEMBA</b>	<b>115,000,000</b>	<b>140,000,000</b>	<b>165,000,000</b>
<b>UNGUJA</b>				
<b>KASMA</b>	<b>MAELEZO</b>	<b>MAKADIRIO 2021-2022</b>	<b>MAKISIO 2022-2023</b>	<b>MAKISIO 2023-2024</b>
1422036	Ada ya Uandikishaji wa Vyama vya Ushirika	15,000,000	15,000,000	15,000,000
1422037	Ada ya Ukaguzi wa Vyama na Huduma	15,000,000	15,000,000	15,000,000
1422075	Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira za Nje	290,000,000	490,000,000	590,000,000
1422011	Vibali vya Kazi kwa Wataalamu wa Kigeni	1,005,626,000	1,099,592,000	1,006,490,000
1422012	Uthibitishwaji wa Mikataba ya Kazi	800,000,000	1,044,779,000	1,234,779,000
1422071	Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi	595,000,000	660,000,000	806,000,000
	<b>JUMLA UNGUJA</b>	<b>2,720,626,000</b>	<b>3,324,371,000</b>	<b>3,667,269,000</b>
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>2,835,626,000</b>	<b>3,464,371,000</b>	<b>3,832,269,000</b>